# Nipashe

Ijumaa Julai 24, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580292

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## CHADEMA yajifungia kuwajadili wanachama waliotia nia urais

UKURASA 3


Ubaguzi, matusi havituachi salama

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ununuzi wa mafuta kwa pamoja umezaa kanuni ya uchumi kitaifa

Wizara yawashika mkono wananchi Mkuranga kuingia ufugaji wa kisasa


• Vita kuukabili 'mdondo', kulinda nyama nyeupe

UKURASA 11

# Moto wa JPM wawaponza vigogo tisa TAKUKURU

## WASIMAMISHWA

kupisha uchunguzi, tume huru yaundwa kubaini madudu gharama za ujenzi...*Endelea uk. 2*




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo, akizungumza jijini Dodoma jana, wakati akitangaza kuwasimamisha kazi watumishi tisa, kupisha uchunguzi kuhusu ujenzi wa majengo saba ya taasisi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## MCHUANO WA VITI MAALUM UBUNGE CCM WASHIKA KASI

UKURASA 3

# NEC yafungua pazia la urais, ubunge, udiwani

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** EYMAEL AKERWA, KATWILA KUJIUZULU UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# NEC yafungua pazia fomu urais

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetoa ratiba ya uchukuaji fomu za kugombea nafasi ya urais, ubunge na udiwani nchini, huku ikibadili majina ya majimbo matatu.

Mwenyekiti hiyo, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alitoa taarifa hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kutokana na uteuzi wa wagombea wa urais, ubunge na udiwani kufanyika Agosti 25 mwaka huu, uchukuaji wa fomu za kugombea kiti cha Rais utaanza Agosti 5 hadi 25 mwaka huu katika ofisi za NEC zilizoko Njedengwa jijini hapa.

"Wagombea wa nafasi ya ubunge na udiwani fomu zitaanza kutolewa Agosti 12 hadi 25 mwaka huu kwenye makao makuu ya halmashauri na kata husika na kampeni za uchaguzi kwa nafasi zote zitafanyika kuanzia Agosti 26 hadi Oktoba 27 mwaka huu," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi wenye sifa za kuwania nafasi hizo ambao watakuwa wamependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu, wajitokeze kuchukua fomu kwa kipindi hicho.

Alitaja kubadilishwa kwa majina ya majimbo matatu ambayo ni Chilonwa litakaloitwa Chamwino, Mtera litaitwa Mvumi na Kijito Upele lililoko Mjini Magharibi, litaitwa Pangawe.

Alitangaza idadi ya majimbo kuwa ni 264 kama ilivyokuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Kati yake, 214 yako Tanzania Bara na 50 yako Zanzibar na kata 3,956.

"Kwa mujibu wa ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tume imepewa jukumu la kuchunguza na kuigawa mipaka kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge.

Vilevile, Ibara ya 74 inasema tume inaweza mara kwa mara au angalau baada ya miaka 10 kuchunguza mgawanyo wa Jamhuri katika majimbo," alisema.

Alisema kuwa tume kwa kutumia mamlaka hayo haikuchunguza, wala kugawa majimbo mapya kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Linapokuja suala la kubadili majina maombi yanakuwa yameletwa kwenye tume na yamepitishwa kwenye vikao vya tume na tume inakuwa tayari imetoa uamuzi, Rais inawezekana alikuwa jana hajapata taarifa ya mabadiliko ya majina, lakini vikao vya tume tayari vimeshafanya vikao na tayari vilisharidhia mabadiliko hayo," alifafanua.

**KAULI YA CUF, NCCR**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Antony Komu, akizungumzia ratiba ya NEC, aliiambia Nipashe jana kuwa chama chake kimeridhia ratiba hiyo na kusisitiza tume ihakikishe inasimamia utekelezaji wake.

"Sisi tumeiona ile ratiba na hatuna tatizo nayo, isipokuwa shida ipo kwenye utekelezaji wake. Kutoa ratiba ni jambo moja, lakini kuisimamia ni jambo jingine.

"Siku 60 ni 'reasonable' (zinatosha) hasa kulingana na hali yenyewe hii ya ugonjwa wa corona. Sisi tunaomba tu waiishi hiyo ratiba na hatutaki yajirudie kama ilivyotokea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Chama cha Wananchi (CUF) nacho kimesema kimeipokea ratiba hiyo kwa mikono miwili na kwa sasa hakioni tatizo ndani yake.

"Sisi kama CUF hatuna tatizo na ratiba iliyotolewa na NEC, tumeipokea," alisema Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai.

**Imeandikwa na Augusta Njoji, Dodoma na Elizabeth Zaya, Dar**



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, akizungumza jijini Dodoma jana, wakati akitangaza ratiba ya uchukuaji wa fomu kwa wagombea urais na majimbo kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Moto wa JPM' waponza watumishi 9 TAKUKURU

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli, kushtuka na kuhoji gharama kubwa za ujenzi wa majengo ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), taasisi hiyo imechukua hatua na kuwasimamisha kazi watumishi wake tisa.

Taasisi hiyo imewasimamisha kazi watumishi hao wa kitengo chake cha Usimamizi wa Miliki ili kupisha uchunguzi wa ujenzi na usimamizi wa majengo mapya saba ya taasisi hiyo.

Majengo hayo yamejengwa katika wilaya za Chamwino na Mpwapwa (mkoani Dodoma), Ngorongoro (Arusha), Manyoni (Singida), Masasi (Mtwara), Namtumbo (Ruvuma) na Ruangwa (Lindi).

Juzi Rais Magufuli aliibana taasisi hiyo kuhusu gharama za ujenzi wa ofisi ya Chamwino, mkoani Dodoma ambapo, alisema kwa mwonekano wa jengo la ofisi hiyo ilitakiwa kugharimu Sh. milioni 40 badala ya Sh. milioni 143.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema uchunguzi huo utafanyika ndani ya siku saba ili kupata ukweli kama kuna ubadhirifu au wizi katika ujenzi huo.

Aliwataja watumishi waliosimamishwa ni Juhudi Nyakongeza, Adam Mandia, Fortunatus Ngailo, Mohamed Kichewele, Nathaniel Otieno, Wilhelm Chuwa, Hamis Masoud, Mbwana Malumbo na Benedict Mabula.

"Nimechukua maamuzi ya kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi watumishi wote waliohusika na usimamizi na ujenzi wa majengo haya," alisema.

Alisema ameunda kamati huru kutoka nje ya TAKUKURU yenye watu wanne itakayoanza kazi rasmi ya siku saba kuanzia Julai 27, mwaka huu.

Alisema tuhuma zozote zitakazobainika na kuthibitika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Kutokana na kauli hiyo ya Rais nimeamua kuchukua hatua tatu za haraka ambazo ni kuunda kamati huru, kusimamisha wahusika na kuvunja kitengo cha miliki TAKUKURU ili kisukwe upya," alisema Brigedia Jenerali Mbungo.

Aidha, Mkurugenzi huyo alisema kamati itakuwa na mtaalamu kutoka Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na wataalamu wawili kutoka kampuni ya ukandarasi ya SUMA-JKT.

Kwa mujibu wa Mbungo, kamati hiyo itaendelea na uchunguzi wakati watumishi wa kitengo hicho wakiwa nje ya kazi ili ufanyike kwa uhuru bila kuingiliwa na mtu yeyote.

Alisema maagizo ya Rais yalilenga kuondoa viashiria vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wa taasisi hiyo, ambayo imeaminiwa kwa ajili ya kuongoza mapambano dhidi ya rushwa.

Juzi, akizindua ofisi ya TAKUKURU Chamwino ambayo ni miongoni mwa majengo ya aina hiyo saba yalioyojengwa kwenye wilaya hizo, Rais Magufuli aliagiza taasisi hiyo ijitathmini kutokana na gharama kutolingana na jengo husika.

"Huwezi kujenga nyumba kwa Sh. milioni 143, mimi nyumbani nimejenga nyumba ya ukubwa kama huu Sh. milioni 40, tufike mahali tuwe tunazungumza ukweli," alisema na kuongeza:

"Nimehesabu mabati upande huu hayafiki 20, sasa piga upande huu na ule zidisha mara nne, pamoja na kazi kubwa mnayofanya ambayo ni nzuri sana, lazima mjitathmini."

Hata hivyo, alikataa ombi la kufungua majengo hayo saba kwa pamoja, badala yake aliagiza kila jengo litafunguliwa peke yake na viongozi mbalimbali.

Kwa upande wa Mpwapwa atafungua Makamu wa Rais, Manyoni (Spika wa Bunge), Masasi (Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU), Namtumbo (Waziri George Mkuchika) na jengo la intelejensia atafungua Waziri Mkuu.

HABARI KITAIFA

## Sababu kuadimika kwa petroli zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), imetaja sababu zilizochangia kuadimika kwa mafuta ya petroli kwenye baadhi ya maeneo nchini,ikiwemo kuongezeka kwa matumizi yake baada ya kuruhusiwa shughuli zilizokuwa zimezuiwa kutokana na uwepo wa ugonjwa wa corona

Aidha, imesema hivi karibuni zitaingia meli za mafuta ambayo yatatosheleza hadi kipindi cha uchaguzi mkuu 2020.

Akizungumza jijini hapa jana, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema mwezi Juni matumizi ya mafuta yalipanda kwa asilimia saba huku Julai yakipanda kwa asilimia 12.

"Pia tukumbuke hawa waagizaji wanaagiza mafuta kwa miezi miwili ya nyuma, kwa mfano, mafuta ambayo matumizi yake yamepanda kwa mwezi Julai ni mafuta yaliyoagizwa mwezi wa Aprili ambayo yalikuwa yameshuka kwa asilimia saba na shughuli nyingi zilisimama kwasababu ya corona," alisema.

Alisema mfumuko wa biashara ulienda tofauti na mipango ambayo wafanyabiashara walipanga ya uagizaji wa mafuta.



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoa wa Pwani, wakipiga kura za maoni kuchagua wabunge wa viti maalum kwenye makundi matano ya NGO, wasomi, wafanyakazi, walemavu na UWT, mkoani humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanga mgombea urais CHADEMA leo

**Na Mary Geofrey**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), juzi ilikutana jijini Dar es Salaam na kujadili mchakato wa uteuzi wa wagombea urais.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, kamati hiyo pia ilijadili mambo mengine.

Alisema yaliyojadiliwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya ilani za uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, chama hicho leo kitatoa taarifa rasmi ya kina kwa waandishi wa habari juu ya kile kilichojadiliwa.

Makada sita wa CHADEMA wametia nia ya kuwania urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, akiwamo Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu.

Wengine ni Wakili Simba Akaro, Dk. Mayrose Majinge, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, Wakili Gaspar Mwalyela, aliyekuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwitta na Leonard Manyama.

Kwa mujibu wa ratiba ya CHADEMA kuhusu mchakato huo wa uchaguzi, Julai 22 (juzi), Kamati Kuu ilitakiwa kupendekeza jina la mgombea urais ambaye Julai 29 mwaka huu, atapitishwa na mkutano mkuu wa chama.

# Mchuano wa viti maalum ubunge CCM washika kasi

**Na Waandishi Wetu**

KURA za maoni kuwapata wabunge wa viti maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ulifanyika jana katika mikoa mbalimbali nchini kupitia mkutano mkuu maalum wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT).

Mkoani Katavi, aliyekuwa mbunge viti maalum katika Bunge lililopita, Tusker Mbogo, ameongoza kura za maoni kuwania ubunge viti maalumu kupitia CCM.

Mbogo alitangazwa kushika nafasi ya kwanza baada ya kupata kura 120 akifuatwa na Martha Mariki aliyepata kura 110 huku Fortunate Kabeja akipata kura 85 katika nafasi ya tatu.

Uchaguzi huo ulihusisha watia nia 18 wa makundi ya wanawake na wafanyakazi huku kwenye kundi la wafanyakazi, Sikitu Mwangoka akiongoza kwa kupata kura 147 dhidi ya mpinzani wake Neema Tarimo aliyepata kura 17. Tarimo hakuwapo ukumbini.

Mtiania Anna Lupembe alitangaza kujiondoa akisema kuwa ameridhika na matokeo aliyoyapata katika kura za maoni kuwania kuteuliwa kuwania ubunge wa Nsimbo.

Jijini Dar es Salaam, viti maalum vimewavutia makada wa CCM 252 waliojitokeza kutia nia, mkoa huo ukiwa na wajumbe 263 wa mkutano maalum wa uchaguzi.

Makao makuu wa nchi, Dodoma, makada 99 walichukua fomu kuwania nafasi hizo, lakini mmoja hakuwapo ukumbini jana, hivyo kuhesabika kujitoa katika kinyang'anyiro hicho kilichowakutanisha wajumbe 536 kutoa uamuzi.

Katika Mkoa wa Arusha, wajumbe 388 wa mkutano huo walikutana kwenye ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa AICC kuchagua wabunge kupitia makundi matano ya NGOs, wasomi, wafanyakazi, watu wenye ulemavu na UWT.

Pia, wagombea kwa nafasi mbalimbali kutoka majimbo tisa ya mkoa wa Mjini Zanzibar walichuana vikali wakati wa upigaji wa kura hizo kwenye Ukumbi wa CCM, Amani.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja, Maryam Muharami Shomar, alisema kura za maoni zinazoendelea ndani ya Tanzania kwa sasa ni ishara ya safari njema kwa CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu kuendelea kuongoza dola.

Katika Bunge la 11, CCM ilikuwa na wabunge wa viti maalum 66, ikiwa ni idadi kubwa zaidi ikifuatwa na Chama cha Demokradia na Maendeleo (CHADEMA) kilichokuwa na wabunge wa viti maalum 37 na Chama cha Wananchi (CUF) kilichokuwa na wabunge wa viti maalum 10.


NMB Karibu yako

MABADILIKO YA MAKATO YA BENKI

**Mpendwa Mteja,**

Benki yako ya NMB inapenda kukutaarifu kuhusu mabadiliko ya baadhi ya Makato kuanzia tarehe 23 Agosti 2020, katika huduma zetu zifuatazo:

| AKAUNTI | MABADILIKO |
|---|---|
| Chap Chap MasterCard | Ada ya Kadi ya Mwaka TZS 9,440 |
| Malipo ya serikali kupitia Wakala | BURE |

NMB Mkononi

ADA MPYA

| Viwango | Ada |
|---|---|
| 1,000 - 4,999 | 950 |
| 5,000 - 9,999 | 1,800 |
| 10,000 - 19,999 | 2,100 |
| 20,000 - 29,999 | 2,700 |
| 30,000 - 49,999 | 4,000 |
| 50,000 - 99,999 | 5,300 |
| 100,000 - 199,999 | 7,100 |

| Viwango | Ada |
|---|---|
| 200,000 - 299,999 | 7,700 |
| 300,000 - 399,999 | 8,300 |
| 400,000 - 499,999 | 9,100 |
| 500,000 - 999,999 | 10,700 |
| 1,000,000 - 5,000,000 | 12,000 |
| Kuangalia Salio | 400 |

Ada za Mwezi

| Akaunti | TZS |
|---|---|
| Akaunti ya NMB Kilimo | 1,800 |
| Akaunti za Biashara (Wateja wadogo na wakati) | 15,340 |

Ada ya TZS 600 kwa miamala iliyo chini ya kikomo cha udhibiti wa akaunti.

Kwa maelezo zaidi tafadhaili wasiliana nasi kupitia namba 0800 002 002 au kwa barua pepe: Hudumakwawateja@nmbbank.co.tz

**Imetolewa na Utawala wa NMB Bank Plc.**

www.nmbbank.co.tz

# Jafo aagiza ujenzi madarasa Temeke

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameiagiza Manispaa ya Temeke kujenga vyumba 20 vya madarasa katika shule nne ili kupunguza msongamano wa wanafunzi.

Pia amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Ludubilo Mwakibibi, kupeleka madawati 300 katika Shule ya Msingi Kizinga, ili kumaliza changamoto ya wanafunzi kukaa chini.

Jafo alitoa maagizo hayo jana katika ziara yake ya siku moja katika Manispaa ya Temeke ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) unaohusisha ujenzi wa barabara za mitaa, ujenzi wa vituo vya afya na masoko.

Akiwa katika shule ya Msingi Mzinga, Jafo alimwagiza mkurugenzi huyo kuhakikisha wanajenga madarasa matano katika shule hiyo na shule za msingi Kongowe, Upendo na Kizinga.

"Naomba nikuagize mkurugenzi mchanga ulipo eneo hili utumike kufyatua matofali ya kujengea madarasa matano hapa na shule zingine za Kongowe na Upendo, lengo tupunguze msongamano wa wanafunzi madarasani," alisema Jafo.

Kadhalika aliagiza kusafishwa kwa eneo la kiwanja cha shule hiyo ambalo kwa takribani miaka mitatu limezungushiwa mabati na kurundikwa mchanga unaofanya wanafunzi wakose eneo la kuchezea.

"Haiwezekani hili eneo limegeuzwa kuwa kichaka cha kuhifadhi vibaka kwa muda wa miaka mitatu ni hatari kwa sababu watoto wetu wanaweza wakabakwa, wakati mchanga huu ungeweza kutumika kujenga madarasa ya kusomea wanafunzi," alisema Jafo.

Akiwa katika Shule ya Msingi Kizinga, Jafo alimwagiza mkurugenzi huyo kutengeneza madawati 200 hadi 300 ndani ya wiki tatu na kuyakabidhi shuleni hapo ili kumaliza upungufu huo unaofanya wanafunzi kukaa chini.

Jafo pia alitembelea ujenzi wa barabara ya Mwera Mbagala yenye urefu wa Kilometa 7.5 inayojengwa na mkandarasi wa ndani Jasco ambayo ujenzi wake umefika asilimia 42 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba.

Jafo alitembelea Zahanati ya Buza ambayo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.9 na itaanza kufanya kazi muda mfupi baada ya kuwekewa vifaa vyote ya kutolea huduma za matibabu.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, alimpongeza Waziri Jafo kwa kazi kubwa anayoifanya na kuahidi kuwa atatekeleza maagizo yote aliyotoa katika wilaya hiyo ili miradi yote ikamilike kwa wakati.

# Wanafunzi elimu ya juu walia posho kufyekwa

**Na Romana Mallya**

MTANDAO wa Wanafunzi Tanzania (TSNP), umeilalamikia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kukata fedha za kujikimu bila kushirikishwa.

Hata hivyo, bodi hiyo imesema imetoa fedha hizo kulingana na siku za masomo vyuoni na kupungua kwa posho hizo kunakolalamikiwa, kumetokana na idadi ya siku za masomo kupungua pia.

Katibu wa TSNP, Robert Sylivester, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa posho ya kujikimu kwa mwaka huu wa masomo (2019/20) imepungua huku ada ya masomo ikiendelea kubaki kama ilivyo licha ya wanafunzi kukaa nyumbani kwa takriban miezi mitatu wakati wa mlipuko wa corona.

Sylivester alisema wameshangaa kuona bodi imewakata fedha za kujikimu bila kuangalia mahitaji yaliyoongezeka kutokana na mlipuko wa virusi hivyo.

"Mei 21, mwaka huu, bodi ilitoa ufafanuzi kuwa malipo yote kwa wanufaika yatafanyika kama hapo awali na fedha za wanufaika zipo na tayari walikuwa wameshaanza mchakato wa kuzifikisha kwa walengwa. Kama kulikuwa na mabadiliko, yangewekwa wazi mapema," alisema.

Sylivester alihoji kwa nini fedha za ada zimelipwa zote vyuoni bila kupunguzwa licha ya siku za masomo kuwa chache.

Alisema bodi ilipaswa kutoa taarifa mapema kwao baada ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoa mwongozo kwa elimu na vyuo kuwasilisha ratiba zao.

"Uhalisia wa fedha za chakula na malazi kwa sasa haukidhi mabadiliko ya kimfumo na kimaisha yaliyochagizwa na ugonjwa wa corona, tunahitaji vitakasa mikono, barakoa na usomaji wa mtandao," alisema.

Kutokana na hilo, mtandao huo umeitaka bodi kutoa ufafanuzi yakinifu na wa haraka, ikizingatia mikataba baina yao na wanufaika, irejeshe fedha zilizokuwa awali na kuhakikisha inakuwa na utaratibu shirikishi.

Hata hivyo, Nipashe ilipoitafuta bodi kuzungumzia suala hilo, uongozi wake ulisema ulipaji wa fedha hizo umetokana na baadhi ya vyuo kupunguza siku za masomo.

"Baadhi ya vyuo vimepunguza siku za masomo kutoka siku 60 wengine wametuandikia barua kutujulisha kuwa wamezipunguza hadi siku 40 kwa hiyo tulichofanya tumelipa fedha za kujikimu kulingana na siku ambazo wanafunzi watakuwa vyuoni.

"Kwa siku huwa tunalipa Sh. 8,500. Kwa hiyo, kama chuo kimepunguza siku za masomo tunapiga mara idadi ya siku zilizobaki ndiyo tumelipa. Baadhi ya vyuo vilivyotuandikia kupunguza siku ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

"Vyuo vilipofunguliwa baada ya corona, tulilipa malipo ya robo ya tatu ambapo robo ya nne inatakiwa ianze Juni Mosi kwa siku 60 ambapo Julai 30 ilikwisha.

"Malipo ya robo ya nne ya mwisho yanayotakiwa kuanza Agosti Mosi, baadhi ya vyuo vimebadilisha ratiba zao na kutuarifu," bodi hiyo iliiambia Nipashe jana.




Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) Taifa, Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), akipokea fomu kutoka kwa Katibu wa Jumuiya ya Vijana ya Wilaya ya Ilala, Salum Seleman, ili kuteuliwa kugombea urais. Katikati ni Katibu Mkuu wa Chama hicho, Haroubu Shamisi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vijana CUF wamchukulia fomu urais Prof. Lipumba

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, ameridhia ombi la vijana wa chama hicho walilomuomba agombee nafasi ya urais kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao.

Profesa Lipumba alipelekewa fomu na vijana wa chama hicho kutoka katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam katika ofisi zake makao makuu ya chama hicho yaliyopo Buguruni, Ilala jijini Dar es Salaam.

Vijana hao walisema wameamua kumpelekea fomu hiyo kwa sababu wanaamini yeye ndiye atafaa zaidi kupeperusha bendera ya chama hicho katika nafasi hiyo ya urais.

Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa CUF Taifa, Juma Kilaghai, alisema gharama ya fomu ya kugombea nafasi hiyo ndani ya chama hicho ni Sh. 500,000 na kwamba vijana hao walichangishana na kupata fedha hiyo na kumchukulia Mwenyekiti wao fomu.

"Baada ya kuona Mwenyekiti yuko kimya, vijana wa chama chetu kutoka katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, walijikusanya kujichanga kwa ajili ya kupata fedha ya kuchukulia fomu na baada ya kufanikiwa, jana (juzi) walimuandikia ujumbe mfupi kupitia simu yake ya mkononi kuomba kukutana naye saa nne asubuhi ofisini kwake," alisema Kilaghai.

"Mwenyekiti alikuwa Dodoma, lakini akakubali kuja kuwasikiliza, na leo wamekuja kumuomba akubali kuchukua fomu hiyo, wamemkabidhi na amekubali kuchukua fomu na kuijaza kwa ajili ya kuomba kuteuliwa kupeperusha bendera ya chama."

Akizungumza baada ya kupokea fomu hiyo kutoka kwa vijana hao, Profesa Lipumba alisema alichelewa kuchukua fomu hiyo ili kutoa fursa kwa wanachama wengine kufanya hivyo. "Sikutaka kuchukua fomu haraka kwa sababu nilitaka kutoa fursa kwa wanachama wengine kufanya hivyo, unajua watu wengine wakiona nimechukua mimi wangeogopa kuchukua," alisema Profesa Lipumba.

Profesa Lipumba alisema miongoni mwa vipaumbele vyake endapo atateuliwa na chama chake kuwania nafasi hiyo na hatimaye chama chake kushika dola ni pamoja na kuunda serikali ya umoja wa kitaifa. Profesa Lipumba alisema atahakikisha serikali yake inakuwa jumuishi kwa wananchi walio kwenye vyama vya siasa na wasio na vyama vya siasa.

Pia alisema atahakikisha serikali yake inayapa kipaumbele mambo ya msingi ya kitaifa na kuyashughulikia kwa nguvu zote.

# Zimamoto yaomba ujenzi visima mitaani

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JESHI la Zimamoto na Ukoaji nchini limeziomba mamlaka zinazohusika na usambazaji maji katika maeneo mbalimbali ya wananchi nchini kujenga visima mitaani ili kuliwezesha jeshi hilo kupata huduma hiyo kwa urahisi na kukabiliana na majanga ya moto kwa wakati.

Kauli hiyo imetolewa jana na Kamshna Jenerali wa Jeshi na Uokoaji nchini (CGF), John Masunga, wakati wa ziara yake ya siku moja mkoani Tabora ya kukagua shughuli za jeshi hilo.

Alisema visima vya maji vinapokuwa maeneo mbalimbali na wakati mwingine katika mazingira yasiyofikika kirahisi na magari kunasababisha uzimaji moto kuwa mgumu.

Vile vile, alisema katika kukabiliana na upungufu wa magari, wameingia makubaliano na Shirika la Nyumbu ambalo ni la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) la kuwatengenezea magari ya kuzimia moto.

CGF Masunga alisema magari hayo yanatarajiwa kukamilika katika muda mfupi na yatakapokamilika watayasambaza kwenye mikoa mbalimbali ili yaweze kusaidia kuongeza vitendea kazi.

Alitoa wito kwa jamii kutoa taarifa mapema kwa Jeshi hilo pindi wanapokabiliwa na majanga ya moto, barabarani, majini ili waweze kupata msaada.

Katika hatua nyingine alimshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa kulipatia Jeshi hilo Sh. bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa magari ya askari wa Jeshi hilo.

Alisema ujenzi wa nyumba za makazi ya askari wa Jeshi hilo umeanza na wameanzia mkoani Dodoma na kuwapo kwa ongezeko kubwa la askari kwa sababu ya kuhamia makao makuu ya nchi.

Kuhusu makazi ya askari wa mikoani, amewaagiza makamanda wa mikoa yote kuongea na halmashauri kwa ajili ya kupata viwanja vya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora Dk. Philemon Sengati, alilishukuru Jeshi hilo mkoani humo kwa juhudi za kukabiliana na majanga mbalimbali.

Alisema ofisi yake itaendelea kushirikiana na Jeshi hilo kuzuia na kukabiliana na majanga yanapotokea.

# Makabe, Msakuzi walia usafiri

**Na Fatma Mtutuma,** UDOM

WATUMIAJI wa vyombo vya usafiri eneo la Mbezi Makabe Msakuzi, wameiomba serikali kutengeneza barabara hiyo ili kuwaondolea usumbufu na uharibifu wa mali.

Ubovu wa barabara hiyo umesababisha usafiri kuwa mgumu hasa nyakati za asubuhi na jioni, muda ambao watu wengi wanaondoka na kurudi nyumbani.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya watumiaji, Vailet Jekap na Neema John, walisema ubovu wa barabara ni moja ya sababu zinazochangia usafiri kuwa mgumu hasa kwa wanafunzi.

"Muda tunaotoka shule hadi kufika nyumbani huwa tunakaa sana hapa kituoni, hii ni changamoto ya barabara pia hata yatakapofika hapa msongamano wa watu ni mkubwa sana na magari hayo hayana uwezo wa kubeba hata zaidi ya watu 20," alisema Jekapu.

Aliongeza: "Tunafika nyumbani usiku sana muda ambao tulitakiwa tuwe tushafanya kazi zingine na kujisomea masomo yetu na kujiandaa kwa ajili ya kesho."

Mmoja wa madereva wa daladala, Fahad Mlole, alisema barabara bado inachangamoto ingawa serikali ilifanya jitihada za kusawazisha kwa kusambaza vifusi.

"Changamoto siyo kwa abiria tu bali hata kwetu sisi madereva, barabara bado haina kiwango kinachofaa ingawa siku za karibuni tuliona vifusi na kusawazisha ilitupa matumaini, lakini mvua iliponyesha hali inarudi kuwa vilevile," alisema Mlole.

"Hali hii inasababisha hata magari makubwa yenye uwezo wa kubeba abiria wengi kituoni kushindwa kuchukua abiria wa Makabe kuhofia kuharibika kwa gari kwa sababu ya barabara hiyo."

Kadhalika, madereva wa bodaboda walisema kazi yao huwa ngumu kutokana na mabonde yaliyo katika barabara hiyo na muda mwingine kusababisha ajali hasa kipindi cha mvua.

# STAMICO yaanza kuchoronga miamba

**Na Sara Magesa, GEITA**

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO), limekuwa la kwanza nchini kunufaika na mabadiliko ya sheria ya madini inayotaka kampuni za uchimbaji madini kutumia makandarasi wa ndani katika kuchoronga miamba .

Hii ni baada ya shirika hilo kutiliana saini mkataba wa kutoa huduma ya uchorongaji na Kampuni ya Uchimbaji ya Dhahabu ya Geita (GGM) wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.6.

Kabla ya mabadiliko ya Sheria ya Madini, GGM ilikuwa ikitumia makandarasi kutoka nje ya nchi kwenye shughuli zake za kuchoronga miamba yenye dhahabu.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba huo iliyofanyika mjini hapa, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alilitaka shirika hilo kufanya kazi kwa weledi na umakini mkubwa wakitambua kazi waliyopewa wakiiharibu watakua wamewaharibia Watanzania.

Waziri Biteko alisema shirika hilo lililoanzishwa toka mwaka 1972 lilikuwa likijiendesha kwa hasara na kuzalisha madeni, lakini toka kufanyika mabadiliko ya uongozi na kuzuia ubadhilifu, limejiendesha na kutoa gawio serikalini.

Alisema iko miradi ya kimkakati ikiwamo kiwanda cha kusafisha dhahabu kwa kiwango cha kimataifa kinachotarajiwa kukamilika Disemba, mwaka huu, kitakachosafisha kilo 480 kwa siku.

Biteko alisema toka kuanzishwa kwake, shirika hilo halikuwahi kuchangia katika mfuko mkuu wa serikali, lakini sasa limeboreka na limetoa gawilo la Sh. bilioni 1.1 kwa mwaka 2019/20.


**The United Republic of Tanzania**

**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**

**NOTICE TO THE PUBLIC REGARDING INDIVIDUALS AND COMPANIES ILLEGALLY OPERATING HOME STAY ACCOMMODATION SERVICES**

It has come to our attention that there are some individuals and companies providing home stay accommodation services to tourists contrary to Section 10, 21 and 31 (sub section 1-6) of the Tourism Act No. 29 of 2008; which requires any person who conducts, operates or intends to conduct or operate a tourism facility or activity to be registered by the Director of Tourism and issued with the Tanzania Tourism Business License (TTBL). Home stay as tourism business activity is guided by The Tourism (Accommodation Facility) Regulations 2015 (GN. No. 498 of 2015) and The Tourism (Fees and Charges) Regulations, 2015 with the amendment (GN No. 506 of 2017).

In view of the foregoing, the Ministry informs all Tourism Agents, Tourism Stakeholders and the general Public that it is against the law to conduct or operate a tourism facility or activity without being registered and licensed. The general Public, Tourists, and Tourism Stakeholders are therefore urged to only trade with companies that are registered and licensed. The list of registered and licensed Tourism Agents for the year 2020 is available in the Ministry's website at the section of stakeholders – Tour Operators.

By this notice the Ministry requires all owners of Home Stays and Tourism Agents in Tanzania Mainland, who are not registered and licensed to be registered and licensed within 30 days from the date of this notice. All applications must be accompanied with the copy of certificate of registration from BRELA, TIN, National Identity Card (NIDA) or travel passport.

For more information, kindly visit our website at www.maliasili.go.tz or visit Headquarter Offices at UDOM, in Dodoma or Tourism Zonal Offices located at Mpingo House - Dar es Salaam; PSSSF – Mwanza, Iringa NSSF Block; and TANAPA Head Quarters in Arusha.

**Issued by:**

**DIRECTOR OF TOURISM**
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**
**Tel: +255 712721932**
**Email: dt@maliaisili.go.tz**
**13th July, 2020**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kipenga cha uchaguzi kimepulizwa, wagombea wafuate sheria, taratibu

**KIPENGA** cha uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kimepulizwa rasmi, baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza jana kuwa uchukuaji wa fomu za wagombea udiwani na ubunge zitaanza kutolewa Agosti 12 hadi 25 mwaka huu.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Semistocles Kaijage, akizungumza na waandishi wa habari habari jijini Dodoma jana, a lisema kutokana na uteuzi wa wagombea wa urais, ubunge na udiwani kufanyika Agosti 25, mwaka huu, uchukuaji wa fomu za kugombea kiti cha urais zitaanza kutolewa kuanzia Agosti 5 hadi 25, mwaka huu katika Ofisi za NEC jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Jaji Kaijage, wagombea ubunge na udiwani watapaswa kuchukua fomu kwenye makao makuu ya halmashauri na kata husika, na kwamba kampeni za uchaguzi kwa nafasi zote zitafanyika kuanzia Agosti 26 hadi Oktoba 27, mwaka huu.

Alitoa wito kwa wananchi wenye sifa za kuwania nafasi hizo ambao watakuwa wamependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu wajitokeze kuchukua fomu kwa kipindi hicho.

Mbali na kueleza kwa undani kuhusu ratiba hiyo, mwenyekiti huyo wa NEC alisema alibainisha kubadilishwa kwa majina ya majimbo matatu ambapo Jimbo la Chilonwa ambalo litaitwa Chamwino. Jimbo la Mtera litaitwa Mvumi na Kijito Upele lililopo Mjini Magharibi litaitwa Pangawe.

Kwa mujibu wa Jaji Kaijage, idadi ya majimbo ni ni 264 kama ilivyokuwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, ambapo 214 yapo Tanzania Bara na 50 yapo Zanzibar pamoja na kata 3,956.

Tangazo hilo la NEC linaashiria kuwa sasa vyama vyote vya siasa nchini vyenye usajili wa kudumu vina fursa ya kushiriki baada ya kukamilisha uteuzi wa wagombea wao na kuwasilisha majina yao kwenye tume.

Hilo ni takwa la kisheria na kikanuni kwa kuzingatia kuwa sheria ya uchaguzi inaelekeza kuwa wagombea wote wa nafasi za kisiasa lazima watoke kwenye vyama vya siasa.

Hivyo kwa mujibu wa sheria, hakuna raia wa Tanzania anayeweza kugombea nafasi ya kisiasa kuanzia ngazi ya vitongoji, mitaa, vijiji, kata, jimbo hadi taifa bila kupitia chama cha siasa, ambacho ndicho mdhamini wake.

Wakati NEC ikitangaza ratiba ya mchakato wa uchaguzi huo ambao utafanyika Oktoba 28, vyama kadhaa vimeshaanza michakato ya kupata wagombea wa ngazi zote kupitia kura za maoni.

Kila chama kinachokusudia kushiriki uchaguzi huu ni wakati wa kuharakisha na kukamilisha mchakato wa kuteua wagombea ili kuwahi ratiba ya tume ya uchukuaji wa fomu.

Kadhalika, vyama vya siasa vitatakiwa kuhakikisha kuwa vinawasimamia na kuwaongoza wagombea wake katika kukamilisha masharti yanayotakiwa ya ujazaji wa fomu kabla ya kuziwasilisha NEC kwa ajili ya uteuzi.


Itakumbukwa jinsi Novemba mwaka jana wakati wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa yalivyozuka malalamiko mengi baada ya wagombea wengi wa vyama vya upinzani kukosa uteuzi kwa madai kuwa walishindwa kujaza fomu.

Ni sababu hizo zilizosababisha vyama kadhaa kususia uchaguzi huo na kuacha mjadala mpana. Hata hivyo, tusingependa hali hiyo ijitokeze tena mwaka huu.

Tumaanini pia kuwa vyama vya siasa vitateua wagombea wenye sifa zinazokubalika kikatiba, kisheria na kikanuni, hivyo kuepuka kuenguliwa na NEC wakati wa uteuzi wa wagombea.

Tusingependa kusikia michakato ya uteuzi wa wagombea ndani ya vyama inaibua migogoro, migongano na mitafaruku ambayo haina tija kwa taifa na kwa vyama vyenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Mbinu hizi mbili muhimu kukabili janga la saratani

**CHANZO** kikubwa cha watu kukumbwa na saratani mbalimbali zikiwamo za koo, ngozi na nyingine nyingi, ikiwamo mlo: Kimsingi, ulaji kwa kanuni duni una hatari kubwa.

Inaelezwa kuwa ni muhimu watu kufuata kanuni bora za lishe, ili kuepuka kukumbwa na ugonjwa huo hatari na pia kuwa tayari kufuatilia ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaselage, anasema saratani ya shingo ya kizazi inaongoza kwa wagonjwa wengi, huku jijini Dar es Salaam, saratani ya matiti ndio kinara,

Nyingine zinazotajwa kuwasumbua Watanzania ni saratani za koo, ngozi, matezi, damu, kibofu cha mkojo na tezi dume, ambazo cha muhimu kinachohimizwa juu yake ni umuhimu wa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya.

Hadi sasa imeshawekwa wazi kuwa utoaji huduma za matibabu ya ugonjwa wa saratani upo katika hospitali zote nchini, lengo ni kurahisisha mawasiliano kati ya madaktari bingwa na wataalamu wengine wa saratani.

Hapo kuna mawili muhimu yanayopaswa kuzingatiwa, ili kukabiliana na ugonjwa huo. Kuna sulala la lishe bora, kwenda hospitalini na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya.

Ni bahati mbaya, baadhi ya watu huwa wazito kuzingatia lishe bora inayohusisha ulaji mboga za majani ambazo wengi wanazipuuza, wakiangukia mbadala kama chipsi vingine vinavyofanana navyo

Inaelezwa kuwa vyakula ambavyo baadhi ya watu wanavidharau, ndivyo vinavyofaa kwenye afya. Hivyo, kuna haja ya kubadilika kwa kuacha kula kwa mazoea na kuhamia kwenye miongozo ya lishe bora.

Wavutaji wa sigara ndiyo wanaoelezwa kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na ugonjwa na wapo baadhi yao, kwa kawaida ni wazito kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kuwa mwaka uliopita, kuna wagonjwa wapya saratani duniani milioni 18.1 na kuna wagonjwa milioni 9.6 walipoteza maisha.

Pia, kunatajwa asilimia 70 (sawa na watu milioni 6.7) ya waliopoteza maisha kwa ugonjwa huo wanatoka nchi maskini.

WHO inaelezea umuhimu wa kuongezwa huduma za kukabiliana na saratani katika nchi zenye kipato cha chini na cha wastani.

Wakati kukiwa na juhudi hizo, siyo vibaya jamii pia ikajiongeza kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya, kuanzia ulaji unaotakiwa na hospitalini, kwa ajili ya ushauri na matibabu pale inapobidi.

Njia hizo mbili ni muhimu katika kukabiliana ugonjwa huo, ili kupunguza tatizo hilo, kama siyo kulimaliza kabisa ndani ya jamii, kwa vile linatajwa kuwa watu wa jinsia zote nchini wanaathirika.

Hatua hizo zikichukuliwa, zitasaidia kukabiliana na tatizo hilo, kwani WHO inatahadharisha kwamba bila ya hatua kuchukuliwa, duniani kutashuhudiwa ongezeko kubwa la asilimia 60 ya wagonjwa wa saratani katika miongo miwili ijayo.

Kwani shirika hilo la afya, lina ufafanuzi wake kwamba Takriban ongezeko kubwa kwa kiwango 81 vitatokea katika nchi zenye kipato cha chini, ambako uhalisia ngazi ya kumudu maisha ya kila siku iko chini mno.

Ni ukweli kwamba, iwapo watu wote watazingatia maelekezo ya lishe na kwenda kupata huduma za msingi, kitabibu, saratani inaweza kugundulika mapema, kutibiwa vizuri na wagonjwa wake kupona.

Wataalamu wa afya wameshaweka wazi kuwa ugonjwa huo haupaswi kuwa katika sura ya adhabu ya kifo kwa kila anayepatwa, bali kama ni bahati mbaya ataugua, bado awe na nafasi ya kuhudumiwa baada ya kugundunliwa mapema afike hatua ya kupona.

Hivyo, kushugulikia saratani kwa kuzingatia lishe bora ni jambo muhimu na kwenda kwenye vituo vya afya mapema kupata ushauri wa kitaalamu au matibabu ina ulazima.

## HABARI KITAIFA

# Mwandishi, dereva wahukumiwa kulipa 800,000/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu mwandishi wa habari, Angellah Kiwia na dereva Mohamed Rushaka, kulipa faini ya Sh. 800,000 au kutumikia kifungo cha miaka miwili jela baada ya kukiri na kutiwa hatiani kwa kosa kujipatia pesa kwa njia ya vitisho.

Kadhalika washtakiwa hao wameamriwa kulipa fidia ya Sh. milioni 30 baada ya kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchibi (DPP) ya kukiri makosa dhidi yao.

Washtakiwa Kiwia na Rushaka wamefanikiwa kulipa fedha hizo na wameachiwa huru na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Awali, mahakama hiyo iliwafutia hati ya mashtaka na kuwasomea hati mpya yenye mashtaka matatu.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, aliiomba mahakama kufanyia mabadiliko hati ya mashtaka na katika makubaliano yaliyofanywa baina ya washtakiwa na DPP amewafutia mashtaka ya awali yenye makosa manne na kusoma hati mpya yenye kosa moja la kujipatia fedha kwa njia ya vitisho.

Wakili Komanya aliiomba mahakama kutoa adhabu kulingana na makubaliano yaliyoingiwa kati ya DPP na washtakiwa hao.

Washtakiwa hao walikuwa wanadaiwa kati ya Machi Mosi na Machi 31, 2020 katika maeneo tofauti ya Jiji la Dar es Salaam, kwa makusudi waliongoza genge la uhalifu kwa lengo la kujipatia faida.

Katika shtaka la pili walidaiwa kutenda kosa la utekaji nyara kati ya Machi Mosi na Machi 31, 2020 katika Jiji la Dar es Salaam na kumteka Seleman Mohamed wakiwa na lengo la kumpeleka katika hatari ya kumuumiza.

Pia ilidaiwa katika shtaka la tatu wakiwa na lengo la kulipwa, walidai kiasi cha Sh. milioni 30 kutoka kwa Seleman Mohamed, huku wakimtishia kumuua.

Katika shtaka la nne la kutakatisha fedha, ilidaiwa kuwa washtakiwa hao katika tarehe zilizotajwa awali jijini Dar es Salaam, walijipatia Sh. milioni 30 kutoka kwa Mohamed, huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la makosa tangulizi ya uhalifu.

# Ajali yakatisha maisha ya askari

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

Mtu Mmoja amefariki dunia na wengine wawili wamenusurika kifo baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka.


Mashuhuda wa tukio hilo wamesema kuwa ajali hiyo ilitokea katika kijiji cha Ligunga katika barabara kuu ya Tunduru - Songea na kwamba chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa dereva aliyekuwa akiendesha gari hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 3:50 katika kijiji cha Ligunga watu hao wakiwa njiani kwenda Songea wakitokea Dar es Salaam.

Maigwa alimtaja aliyefariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Askari Polisi Coplo Livinius Ngonyani (54) mkazi wa Ubungo, Dar es Salaam ambaye alisema alikuwa akwenda likizo kwao Songea.

Kamanda Maigwa aliwataja manusura wa ajali hiyo kuwa ni Samson Ngonyani (60) mfanyabiashara mkazi wa Ubungo, Dar es Salaam ambaye ni kaka wa marehemu na dereva ambaye hakutambulika jina ambaye alitoroka baada ya ajali hiyo.

Alisema taratibu za kumsaka dereva huyo zinaendelea na akatumia nafasi hiyo kuwataka wananchi ambao wanazo taarifa za alikokimbilia na kujificha, kutoa taarifa polisi ili akamatwe na sheria kufuata mkondo wake.



# UWT waonywa kununuliwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAJUMBE wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoani Kagera, wametakiwa kutoa hukumu kwa wanachama wake wanaogombea ubunge kupitia viti maalum jinsi wanavyoona badala ya kununuliwa kwa vitenge na kanga.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo, Rashida Mfaume, wakati akizungumza na wajumbe wa UWT kwenye mkutano wa uchaguzi wa kura za maoni za ubunge wa viti maalumu mkoani hapa.

"Chagua wewe mwenyewe unaemtaka sio uliepokea kanga au kitenge chake, hapa tupo kinamama hakuna aliyechaguliwa mume wa kumuoa... na wale watumishi hakuna aliyechaguliwa kazi" alisema Mfaume.

Alisema kila mmoja ana uelewa wake na utashi pia wa kuchagua kiongozi anaemtaka na kuwawakilisha vyema kinamama.

"Hapa anatafutwa atakaewakilisha vyema huko mbele ya safari na atakayeleta maendeleo na manufaa, mnapokea rushwa na nimefika mapema nimeona," alisema Mfaume.

Aidha alisema wawakilishi watakaochaguliwa kwa rushwa watambue watakuwa wamewakosea kinamama mkoani Kagera.

TCCIA Investment Public Limited Company

Millennium Tower II Building 24th floor
P. O. Box 72678 Dar es Salaam

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 22 AGOSTI 2019.**

Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na tano wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 22 Agosti, kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3.00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano ni:**

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano;
2. Kupokea na kuthibitisha mabadiliko kwenye Kanuni za Kampuni;
3. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano;
4. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne;
6. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019;
7. Kupokea na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2019;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 31 Desemba, 2020;
9. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
10. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
11. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano.

**Maelezo:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 10 yatumwe na kumfikia Katibu kabla tarehe 10 Agosti, 2020.
2. Taarifa ya Mwaka 2019 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.tcciainvest.co.tz) na kuanzia tarehe 10 Agosti, 2020.
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa kuteua Mwakilishi atakayehudhuria mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.tcciainvest.co.tz). Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe pkifunguomali@tcciainvest.co.tz au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 19 Agosti,2020.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

Peter W. Kifunguomali
Katibu
20 Julai, 2020

158235

+255 222 701 701 info@tcciainvest.co.tz www.tcciainvest.co.tz

Tccia Investment Plc ©

## Kampuni yaibuka na huduma 'Halikati'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Zantel imezindua huduma maalumu ijulikanayo kama 'Halikati' ili kuwaondolea wasiwasi wateja wake wa kupoteza dakika na vifurushi vya intaneti (MB) pale kifurushi kinapoisha muda wake.

Huduma hiyo ya aina yake inamwezesha mteja kuvusha dakika na MB zilizosalia kutoka kwenye kifurushi cha awali kwenda kifurushi kipya na kumpa uwezo wa kuongea na kuperuzi zaidi.

Akizingumza wakati wa uzinduzi wa ofa hiyo, Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa, alisema huduma hiyo imelenga kuwapa wateja uhuru wa kuchagua kifurushi chochote na kufurahia mawasiliano bila kikomo.

"Mawasiliano ya uhakika ni kiungo muhimu katika kuchochea maendeleo hivyo huduma hii ya 'Halikati' itampa mteja uhakika wa mawasiliano ili kusaidia kuendesha shughuli mbalimbali kama biashara, kilimo na uvuvi bila wasiwasi wa kuisha kwa kifurushi chako," alisema.

Alisema ni dhahiri kuwa shughuli kama kilimo, uvuvi na biashara mbalimbali zikiwamo utalii zinahitaji mawasiliano ili kutafuta masoko, hivyo kuwa na muda wa maongezi na intaneti ni muhimu kufanikisha ukuaji na maendeleo ya shughuli hizo.

Pia alisema huduma hii ya aina yake katika soko la mawasiliano imelenga pia kupunguza kero mbalimbali ambazo wateja wamekuwa wakikumbana nazo ikiwamo wasiwasi wa kuisha kwa vifurushi pasipo kutumia dakika na intaneti.

Naye Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga, alisema kupitia ofa hiyo, Zantel itahakikisha inampa mteja thamani ya pesa kulingana na matumizi yake.

"Hakuna haja ya kusubiri hadi kifurushi chako kiishe, kupitia ofa hii una uwezo wa kununua kifurushi kipya kabla cha awali hakijaisha na ukaweza kuvusha dakika na megabites (MB) zilizosalia," alisema Muga.

HABARI KITAIFA

# Matatani kwa tuhuma za mauaji ya mke

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKAZI wa Kijiji cha Biyungu Kata ya Nyabiyonza Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, Alistides Crizostom (40), anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma ya kumuua mkewe, Donina Alistides (53). Naibu Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Issack Msengi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema Julai 21, mwaka huu majira ya usiku, mtuhumiwa alirejea nyumbani kwake na kukuta mkewe akiwa na mwanaume chumbani.

Alisema alipohoji kuhusu mwanaume huyo, Donina hakuweza kujibu ndipo mtuhumiwa alipoanza kumpiga kwa fimbo na kumsababishia kifo.

"Mtuhumiwa aliporejea kwake usiku wa saa 6:00, alikuta marehemu akiwa na mwanaume mwingine aliyekuwa akitokea chumbani, aliuliza hakuweza kumjibu ndipo alianza kupiga na fimbo nyingi hadi kuumua," aliongea Msengi.

Kaimu Kamanda Nsengi alisema, chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi, na kubainisha kuwa baada ya mtuhumiwa kufanya mauaji siku iliyofuata mwili wa marehemu ulikutwa umetupwa shambani.

Mtuhumiwa anashikiliwa na Jeshi la Polisi, na kwa mujibu wa Nsengi, upelelezi ukikamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.




Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi (kulia), akijadiliana jambo na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Tanga, Amir Mruma, akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua shughuli mbalimbali zinazofanywa na mahakama, mkoani Tanga jana. **PICHA: LYDIA CHURI**

# Watumishi mahakama wakumbushwa weledi

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, amewataka watumishi wa Mahakama ya Tanzania kufanya kazi kwa kujituma, kujitolea, na kushirikiana.

Akizungumza na watumishi wa Mahakama ya Wilaya ya Kilindi jana wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani humo, Jaji Kiongozi pia aliwataka watumishi hao kuzingatia maadili wanapotekeleza majukumu yao ili kujenga taswira chanya ya mahakama kwa wananchi.

"Ombeni kupewa kazi za ziada kwa viongozi wenu pale mnapoona kituo husika hakina mashauri mengi, hata kumsaidia hakimu mfawidhi kufanya utafiti ili kurahisisha kutoa maamuzi kwa wakati au vituo vya jirani ili kuboresha utendaji," alisema Jaji Kiongozi.

Jaji Feleshi aliwashauri watumishi kuanzisha vikao vya kitaaluma ili kujengeana uwezo katika fani zao. Alisema sheria na kanuni zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara hasa kwa miaka ya hivi karibuni ikiwamo sheria ya mwenendo wa madai na sheria za mahakama za mahakimu ili kutafuta na kupata ubobezi kwenye taaluma.

"Hakuna hakimu wa mjini wala wa kijijini wote nyinyi ni wamoja kwenye suala la kutafsiri sheria zilizotungwa na Bunge na kanuni zake, vikao hivi vitawasaidia kuwajengea uwezo na uelewa wa kuendesha shughuli zenu za kila siku za utoaji haki kwa wananchi." alisisitiza Jaji Kiongozi.

Jaji Feleshi aliwahimiza watumishi kuzingatia maadili, kufanya kazi kwa bidii, na kuonyesha uadilifu kwa vitendo waendelee kutenda haki. Aliwataka viongozi kusimamia kikamilifu na kutumia busara katika kulea, kuonya, kutoa ushauri na kueleza ukweli.

Aidha, Jaji Feleshi pia aliwataka viongozi kusimamia masuala yote yanayowahusu watumishi na kuyapa kipaumbele ikiwa ni pamoja na kujenga mahusiano mazuri mahala pa kazi, kuzifahamu changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati. Aliongeza kuwa endapo viongozi watakuwa wakiwaelimisha watumishi haki zao za msingi watasaidia kuondoa malalamiko yasiyo ya msingi.

Aliwataka watumishi kuendelea kuwahudumia wateja bila kuchoka na kuacha kutumia lugha zisizofaa. Wadau wetu wengi mara nyingi wanapofika mahakamani huwa na mitazamo tofauti hivyo wakieleweshwa wataelewa na kuondoa migongano na manung'uniko yasiyo ya lazima," alisema.

Wakati huo huo Jaji Kiongozi alikutana na Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Sauda Mtondoo, ofisini kwake na viongozi wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya na kufanya mazungumzo, ambapo mkuu huyo wa wilaya aliishukuru Mahakama ya Tanzania kwa kuanzisha Mahakama ya Wilaya ya Kilindi baada ya maombi ya muda mrefu.

Akizungumza na Mkuu huyo wa Wilaya, Jaji Kiongozi alisema mahakama kwa sasa imejiimarisha na inasisitiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kurahisisha shughuli zake za kila siku za utoaji haki.

"Mfumo huu umesaidia kurahisisha uendeshaji wa mashauri na kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa kwa upande wa wadau na Mahakama, hivyo tembeleeni mifumo ya Mahakama ili kujua mambo mengi yanayofanyika," alisema.

Jaji Kiongozi pia alitembelea eneo linalojengwa Mahakama ya Wilaya ya Kilindi na kupokea taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la Mahakama hiyo kutoka kwa Mtendaji wa Mahakama ya Tanzania Kanda ya Tanga.

Jaji Kiongozi ameanza ziara ya siku tano Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Tanga ambapo atakagua shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mahakama.

# RC aagiza TANESCO, VETA kumaliza suala kuunganishiwa umeme

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA) imetakiwa kukutana na Shirika la Umeme nchini (TANESCO) ili kuangalia njia ya kuondoa kikwazo cha kupeleka umeme katika chuo kipya cha ufundi stadi kinachojengwa wilayani Igunga.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani Igunga na kupata malalamiko kutoka kwa wataalamu wa VETA kuhusu kutopelekwa umeme katika eneo la mradi kwa madai kuwa ni kutokana na gharamu kubwa.

Alisema VETA na TANESCO zote ni taasisi za umma, hivyo ni lazima zikae chini zione kwa jinsi gani zinaweza kutatua mkwamo ambao umesababisha eneo la ujenzi wa chuo lisiunganishwe umeme.

Dk. Sengati alisema kwamba wanaweza wakaona namna nzuri ya kupunguza gharama ili hatimaye umeme ufike eneo la mradi kwa ajili ya kuwawezesha mafundi kufanyakazi usiku na mchana.

Awali Msimamizi wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Igunga, Msabi Masunga, alisema TANESCO iliwapatia hati ya kutaka walipwe shilingi milioni 130, ndipo wawekewe miundombinu ya umeme katika eneo la mradi.

Masunga alieleza kwamba gharama hizo ni kubwa ukilinganisha na fedha ambazo zinatakiwa kukamilisha ujenzi wa chuo hicho ambazo ni shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya majengo mbalimbali na ununuzi wa vifaa.

Aidha, Masunga alisema kuwa katika awamu ya kwanza wamepokea shilingi milioni 250 ambazo zimetumika katika ujenzi wa msingi wa majengo mbalimbali.

Alisema chuo kinatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba mwaka huu, na kuongeza kuwa kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 240 wa kozi za muda mrefu na 500 wa kozi za muda mfupi kwa mwaka.

# Dawa walaji fedha TASAF yapatikana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA kupambana na uingizwaji wa kaya maskini hewa katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kipindi cha pili awamu ya tatu, serikali imeandaa utaratibu wa kuwasainisha mikataba na viapo maalum waratibu wa mpango huo.

Lengo ni kuwawajibisha kisheria watakaobainika katika maeneo yao kuingiza kaya zisizokuwa na sifa.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo na ushirikishwaji makao makuu ya TASAF, Mercy James, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa waratibu wa mradi huo yaliyofanyika wilayani Kahama mkoani Shinyanga, ambayo yanaendana na uhakiki wa kaya za wanufaika wote nchi nzima.

Alisema kuwa awamu hii wamejipanga kuhakikisha wasimamizi wote wanasainishwa mikataba hiyo, ili wanapobainika kwenda kinyume cha mradi kwa kuingiza kaya zisizokuwa na wawajibishwe kisheria, kwamba hatua hiyo itaongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo.

"Zaidi ya kaya 100,000 nchi nzima tunatarajia kuzihakiki na wale watakaokuwa wamekosa sifa tutawaondoa katika mradi huu na tumejipanga kuwajengea uwezo wa kujikwamua kutoka katika hali duni kwa kuwafundisha mbinu za ujasiriamali na ufugaji wa mifugo wa kisasa," alisema.

Aliongeza: "TASAF imejipanga kutoa ruzuku kwa kaya maskini ili kukuza uchumi wao kwa kuhakikisha walengwa wote wanazitumia fedha hizo kama inavyotakiwa ikiwamo katika nyanja za elimu, afya, kilimo na ujasiriamali ili kuleta matokeo chanya katika utekelezaji wa kipindi cha pili awamu ya tatu.

Aidha, alisema kuwa baada ya kukamilika kwa uhakiki, fedha zote za walengwa watapatiwa kwa njia za kibenki au simu za mkononi kupitia akaunti zao, kwamba na hakuna mlengwa atakayepatiwa fedha mkononi kama ilivyokuwa awali ili kudhibiti mianya ya rushwa wakati wa ugawaji.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akifungua mafunzo hayo, alisema serikali imejipanga kuhakikisha wananchi wake wanajikwamua kutoka katika hali duni kwa kuendelea kutoa fedha za TASAF kwa walengwa na kuwataka wasimamizi hao kuwa waadilifu, na kuachana na tabia ya kuingiza kaya zisizokuwa na sifa.

Pia aliwataka waratibu kufanyakazi kwa weledi ili mradi ulete tija na kuongeza kuwa haipendezi kusikia mtumishi amewajibishwa kwa uzembe katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi hasa kwa kuingiza kaya zisizokuwa na sifa kwenye awamu ya tatu.

# NGO zakumbushwa uwazi, uwajibikaji

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO), imeyataka mashirika hayo kuwasilisha taarifa za kila robo mwaka, zinazoonyesha fedha na kazi wanazozifanya kwa msajili ili kujua miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yalipo mashirika hayo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Ofisi ya Msajili wa NGO, Grace Mbwilo, wakati wa ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na mashirika hayo mkoani Iringa.

Mbwilo alisema serikali inafarijika kuona mashirika yanashirikiana nao kufanya kazi za kusaidia jamii na kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo waliopo kwa kufuata taratibu na vipaumbele vilivyowekwa na serikali katika eneo husika.

Ameongeza kuwa mashirika yanapopata fedha nyingi kutoka kwa wafadhili ili kutekeleza miradi mbalimbali ila wanatakiwa kuhakikisha wananchi waliokusudiwa wananufaika na miradi hiyo. "Mwongozo tuliouzindua hivi karibuni unasisitiza uwazi na uwajibikaji kwa sababu tunajua fedha mnaomba kwa ajili ya Watanzania, hivyo ni wajibu wa serikali na jamii husika kufahamu zinafanya nini za zimeleta matokeo gani," alisisitiza.

Aidha, alibainisha kuwa kwa sasa NGO na serikali zinashirikiana, hivyo kuyasihi mashirika kutotumia njia za mkato, kwani watachelewa kufanya kazi zao, hivyo kukwamisha kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa wakati.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Msajili wa NGO, Jaina Said, alisisitiza mashirika kufuata sheria na taratibu zilizopo kwa kutochelewesha taarifa muhimu zinazohitajika kuwasilisha na mashirika hayo katika Ofisi ya Msajili na kusubiri faini.

"Wengine wanaona faini ni hela ndogo, tunakupiga faini kukumbusha wajibu wako, lakini ikiwa ni zaidi ya mara moja tunakuangalia vizuri kama unafaa," alisema Jaina.

Hata hivyo timu hiyo imelipongeza Shirika la Ilula Orphanage Program (IOP) kwa miradi yenye lengo la kusaidia jamii hasa katika kusomesha watoto wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Akielezea utekelezaji wa Miradi ya IOP, Katibu Mtendaji wa Shirika hilo, Edson Msigwa, alisema shirika lake linafanya shughuli mbalimbali za kusaidia jamii ikiwamo kulea na kusomesha watoto, kujenga madarasa na kuwezesha wananchi kiuchumi.

"Shirika letu lina miradi zaidi ya 20 na kubwa tunajishughulisha na kusomesha watoto ambao ni yatima na wanaoishi katika mazingira magumu na tayari watoto 2000 wamenufaika na mradi huo," alifafanua.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ilula, Joyce Michael, alilishukuru IOP kwa kukarabati madarasa mawili shuleni hapo, hivyo kupunguza msongamano wa wanafunzi ambao ungeweza kusababisha kushuka kwa kiwango cha elimu.



Ofisa Programu Msaidizi wa Idara ya Habari ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jackson Malangalila, akiwafundisha wanawake wanaofanya biashara nje ya mipaka ya Tanzania, jinsi ya kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa ajili ya kuboresha biashara zao, wakati wa semina ya kuwajengea uwezo, iliyoandaliwa na mtandao huo, jijini Dar es Salaam, jana.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Vijana Igunga waonywa kushinda vijiweni

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

VIJANA wilayani Igunga Mkoa wa Tabora, wametakiwa kutumia fursa ya miradi mikubwa mitatu ya maendeleo kujiajiri wenyewe kwa ajili ya kuondokana na umaskini na kujipatia kipato.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, wakati wa ziara yake wilayani Igunga ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema vijana wa Igunga hawana sababu za kushinda vijiweni kwa sababu wanazo fursa za kilimo, ufugaji na ufundi ambazo zinaweza kubadili maisha yao na wilaya kama wataamua kuzitumia ipasavyo.

Aliitaja miradi ya kilimo cha umwagiliaji ya Mwamapuli, miradi ya ufugaji wa samaki kutokana na uwapo wa vifaranga vingi vya samaki vinavyozalishwa katika Kituo cha Kanda Ukuzaji Viumbe Maji-Mwamapuli kilichopo Igunga na kujiunga na kozi za ufundi stadi.


Dk. Sengati alisema kwamba vijana wa Igunga hawana sababu za kulalamika kuwa hakuna ajira na kubaki maskini kwa kuwa Igunga inayo mashamba makubwa na maeneo mengi ambayo yanaruhusu kilimo cha umwagiliaji. Dk. Sengati alisema fursa nyingine ni pamoja na kutumia vizuri uwapo wa Kituo cha Kanda Ukuzaji Viumbe Maji-Mwamapuli kilichopo Igunga kuanzisha ufugaji wa samaki kwa kuwa soko lipo ndani na nje ya nchi.

Aliongeza kuwa ni vema vijana wa Igunga wakachangamkia ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VTC) Igunga kujiunga na kozi ambazo zitawawezesha kujiajiri wenyewe na kujipatia kipato kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Dk. Sengati aliwataka maofisa mifugo wa Wilaya ya Igunga kuhakikisha wanatoa elimu na kuwasaidia wafugaji wa ng'ombe kupata mbegu bora ili waweze kuwa na mifugo yenye faida kubwa kwao.

Alisema ng'ombe wengi wanaofungwa katika eneo hilo bei yake iko chini kwa sababu ya kuwa wadogo na kuwa na kilo chache, jambo ambalo halimsaidii mfugaji.

Dk. Sengati alisema ni jukumu la maofisa mifugo kuhakikisha wafugaji wanakuwa na ng'ombe ambao watawasaidia kuwa kipato kikubwa ambacho kitawafanya waishi maisha mazuri, wajenge nyumba nzuri na wasomeshe watoto wao.



Ukurasa 13

Ubaguzi, matusi havituachi salama

BUFE

IJUMAA JULAI 24, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**Ununuzi wa mafuta kwa pamoja umezaa kanuni ya uchumi kitaifa**

# Wizara yawashika mkono wananchi Mkuranga kuingia ufugaji wa kisasa

## • Vita kuukabili 'mdondo', kulinda nyama nyeupe

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

KATIKA kuwawezesha wafugaji kuku wanufaike na bidhaa yao, kanuni inayotawala ni kwamba kuna kila sababu ya kuwapatia mafunzo, wazalishe kwa viwango bora.

Ndani ya mtazamo huo, kuna ukweli unaotawala kwamba wafugaji wanajitokeza zaidi kufuga kuku, lakini wanaishia katika hasara hasa kutokana na mifugo hiyo kufa.

Ili mfugaji aweze kuzalisha kuku bora na wenye afya bora, anatakiwa wapatiwe mafunzo ya ufugaji, kuhakikisha bidhaa hiyo inawainua kiuchumi.

Hadi sasa kuna wafugaji katika mikoa, serikali imeanza kuwapatia mitaji ya kuku na elimu ya kufuga.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, anasema kuwa hadi sasa, serikali inaendelea kuwapatia mafunzo wafugaji kuku, ili wazalishe idadi kubwa ya mifugo hiyo.

Anasema, lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wazalishe kuku bora na wengi, ili kuchangia kusimama kwa uchumi wa nchi, wafugaji wanaendesha shughuli zao kwa tija inayostahili.

Nandonde anafafanua kuwa, ana angalizo la kiuchumi kwamba, inapotokea wafugaji kuku watashindwa kufanya uwekezaji wa nyama nyeupe, inabeba tafsiri ya athari kuwapo eneo la kiuchumi linalochechemea.

"Tumetoa mafunzo ya siku mbili kwa wafugaji kuku kutoka makundi 30 ambayo yanafuga kuku," anasema na kudokeza kuna sehemu ya angalizo la Mpango Kabambe wa Mifugo wa Mwaka 2017 hadi 2021, unaosimamiwa na wizara yenye dhamana na uvuvi kitaifa.

Anasema mtazamo uliopo hivi sasa, ni kwamba mpaka kufikia mwaka 2030, wanalenga kuhakikisha nyama nyeupe inapatikana kwa kiasi kikubwa.

"Bila ya kuwapo elimu yoyote ya ufugaji ifikapo mwaka 2030, nyama nyeupe haitakuwapo na kutakuwapo na upungufu wa nyama (nchini)," anasema.

Anafafanua kuwa, mbali na kutoa elimu ya ufugaji, pia wanasambaza elimu itakayosaidia kuwahudumia kuku watakapokuwa wanaumwa.

Nandonde anasema, hadi sasa wizara yake imeshaanza kuzalisha dawa za chanjo za kuwasaidia wafugaji, hasa panapoibuka magonjwa ya mdondo.

Mkurugenzi huyo anasema, mdondo una kawaida ya kuwakumba kuku kila mara, lakini kukosa elimu kwa wafugaji wamekuwa wakitumia mbinu potofu ya kuwapatia kuku majani, wakidhani kuwa ni dawa mbadala.

Kwa mujibu wa Nandonde, mradi hadi sasa unaendelea kujikita kutoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Dodoma, Singida na wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani.

Anadokeza kinachofanyika sasa ni mkakati wa kugawa bure kuu kwa vikundi vya wafugaji, ikiwa ni namna ya kuinua hamasa za ufugaji katika jamii, Mkuranga ukiwa mfano mojwapo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ullega, anasema mwaka jana walikabidhi kuku kwa baadhi ya watu, lakini walipowatembelea, baadhi hawakukutwa nayo.

"Umekabidhiwa kuku, ni fedha ya serikali. Hivyo, unatakiwa kuwatunza," anasema Ulega, akidokeza ni mwelekeo unaowawajibisha wafugaji wabadilike kiuchumi.

Tahadhari nyingine ya Naibu Waziri huyo ni kwamba kuku hao wasitumike kinyume, ikiwamo kuwachinja.

"Baada ya miezi mitatu tutawatembelea katika vikundi na watakaokutwa wanaendelea vizuri, watapewa kuku mara mbili yake," anasema.

Mary Makolele, ni mfugaji kuku wa Mkuranga, anayewahimiza wenzake kujiunga katika shughuli za ufugaji, kuwaongezea kipato.

Anaipongeza serikali kwa kuwapatia mikopo hiyo ya mifugo isiyo na riba, huku akiwataka wenzake wajitahidi kufuga kwa namna ya kujiongezea kipato na siri ya mafanikio ni kila anayepatiwa mifugo, aisimamie vizuri, ili iwaongezea manufaa ya kipato.



Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde (kulia), akimkabidhi kuku Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, kwa ajili ya kuvipatia vikundi vya wafugaji. **PICHA: YASMINE PROTACE**

UCHUMI

## BOSI WA WAAGIZAJI PETROLI:

# Ununuzi wa mafuta kwa pamoja umezaa kanuni ya uchumi kitaifa

- Achimbua orodha ya mavuno miaka mitano
- Rasmi kwa 'SU'; nchi jirani foleni kujifunza
- Adai bei juu, kukosekana 'sheli' sasa hadithi

**Na Joseph Mwendapole**

MIAKA iliyopita kulisikika malalamiko ya kuwapo gharama kubwa ya mafuta ya petroli, huku kukiwapo matukio ya kukosekana mafuta katika vituo vya kuuzia.

Hiyo iliendana na kushuhudiwa foleni ndefu ya meli zinazopakua mafuta bandarini na hususan, Dar es Salaam, hali iliyosindikizwa na kuyumba bei.

Ni kwanini hiyo? Kuna uamuzi ulifanyika uliokuwa na dhamira ya kukomesha yote hayo. Hatua mojawapo, ambayo ndiyo nuru kuu ya mafanikio mwaka 2015, ilikuwa kubuniwa kwa mfumo wa ununuzi mafuta, maarufu kama 'bulk procurement.'

Umekuwa na mafanikio makubwa katika uchangiaji na ukuaji uchumi, kiasi cha kuvutia nchi jirani kuja kujifunza ili nazo ziweze kuendesha katika mfumo wake wa uchumi.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa (PBPA), Erasto Mulokozi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MKURUGENZI PBPA**

Mkurugenzi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Jumla (PBPA), Erasto Mulokozi, alizungumza na Nipashe, wakati akizungumzia mafanikio ya mfumo huo.

Anayesema mfumo umesaidia kwa kiwango kikubwa uhakika wa mafuta ya kutosha kwa kipindi chote.

Anaeleza mafanikio ya kushushwa gharama za uagizaji mafuta inavyopunguzia gharama kwa mnunuzi wa mwisho, hata kuwavutia majirani Zambia, Uganda, Malawi na Jamhuri ya Kidemorasi ya Congo (DRC) kutuma maofisa wake kujifunza nchini.

Kwa mujibu wa Mulokozi, PBPA inawajibika kuhakikisha nchi inakuwa na mafuta, kwani uadimikaji wa rasilimali hiyo, unaendana na shughuli nyingi za kiuchumi ama kusimama au kusuasua, hata kusababisha taharuki kitaifa.

"Awali waagizaji, yaani kampuni za mafuta zilikuwa zikiagiza kila mmoja kivyake na kila mtu alikuwa akinunua kwa bei yake na akija huku, anauza kwa bei yake," anasema Mulokozi.

Anafafanua hatua iliyochukuliwa, akisema: "Serikali haikuwa na mkono kwenye suala hili hivyo inaona huo siyo utaratibu mzuri ndipo ikazaliwa PBPA."

Mulokozi anaeleza hata taasisi nyingine za serikali zimeanza kuiga mfumo huo wa ununuzi wa pamoja, ikiwamo kwenye mbolea na PBPA imewapa wataalamu wake kuwapa mafunzo ya ununuzi wa pamoja. Anataja mengine, ni mfumo wa kusaidia kupunguza msongamano wa meli, ambazo awali zilikaaa hadi miezi miwili bandarini zikishusha mafuta, jambo lililoongeza gharama za nishati hiyo kwa mtumiaji wa mwisho.

Nchini fani ya ununuzi ambayo imepewa kupaumbele kikubwa, kitaaluma iko chini ya Bodi ya Taifa ya Ununuzi na Usimamizi wa Bidhaa (NBMM) na kuna mamlaka ya udhibiti wa sekta hiyo (PPRA), zote zikitumika kitaifa chini ya sheria inayohusika na ununuzi wa umma.

Mulokozi anaeleza mfumo wa uagizaji huo mafuta uliopigwa katika sehemu nyingi, umeondoa kero kubwa, kwani hivi sasa meli zenye shehena ya mafuta hukaa bandarini kupakua mafuta kwa wastani wa siku tatu.

"Kwa kawaida meli inapozidi kukaa kusubiri kushusha mafuta inatozwa gharama za ucheleweshaji, hivyo wenye kampuni za mafuta walikuwa wakifidia gharama hizo kwa kumwongezea bei mlaji wa mwisho," anafafanua.

**MUSTAKABALI MAFANIKIO**

Mulokozi anarudia kuwa siri ya mafanikio sasa ni mafuta kuuzwa kwa bei nafuu, kuliko ilivyokuwa zamani na nishati imeendelea kuwa chini kwa muda mrefu.


"Tumepunguza msongamano wa meli kabisa, kwa mfano zamani ilikuwa ulete meli tatu, hivi sasa unaleta moja na gharama zinakuwa chini, kulinganisha na zamani kila mtu aliagiza mwenyewe," anasema.

Upande wa gharama za tozo za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mulokozi anaeleza mafanikio ya kupatikana takwimu sahihi za mafuta yanayoingizwa nchini, mamlaka hiyo kujua kodi inayotakiwa kuchukuliwa bandarini, kutokana na mafuta.

Anasema, taasisi nyingine zenye kawaida ya kutoza maji, umeme, barabara na tozo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwenye mafuta, TRA imekuwa ikitumia takwimu hizo kujua kiasi cha fedha wanazotakiwa kupata.



Ushushaji wa mafuta katika Bandari ya Mtwara, ukiendelea.



Msururu wa malori ya kubebea bidhaa za mafuta.

"Mbali na kuisaidia nchi kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingia, pia tuna uhakika wa kuletewa mafuta bora kwa sababu kabla ya meli yetu kushusha mzigo, tunawaita TBS (Shirika la Viwango Tanzania) kuthibitisha na wakitupa majibu, ndipo tunawaambia washushe mzigo," anasema.

Mulokozi anasema ni takwimu zinazoisaidia hata Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kupanga bei elekezi, baada ya kujua gharama halisi za uagizaji mafuta hayo.

Mulokozi anataja kuna baadhi ya vigezo kama bei ya mafuta, gharama za meli iliyobeba shehena na tozo ya meli kuchelewa kushusha mafuta hayo.

Anasema kampuni zinazoagiza mafuta nje ya nchi hivi sasa zimeongezeka kufika 50 na kwamba kadri mahitaji ya nishati inavyozidi kupanda, ni dalili njema kwamba shughuli za kiuchumi zinaongezeka.

**UHABA MAFUTA**

Kuhusu nchi kupatwa na uhaba wa mafuta, Mulokozi anakataa kuwapo uwezekano, kwani wamekuwa wakifuatilia kwa karibu matumizi ya mafuta kila siku na akiba iliyopo kudhibiti uwezekano huo.

Mulokozi anasema sheria iliyopo, inataka kila kampuni ya mafuta iwe na akiba ya mafuta ya kujiendesha kwa walau siku 15, lakini PBPA kupitia kanuni zake inataka kampuni kuwa na akiba ya 40 kukidhi hitaji iwapo shehena zilizoagizwa zimechelewa.

"Meli kutoka Mashariki ya Kati ambako asilimia 70 ya mafuta yetu tunayatoa huko inatumia wastani wa siku 10 au 14 kutegemea na hali ya hewa. Sasa huwezi kujua kitakachotokea, ndiyo sababu tunajitahidi kuweka akiba ya muda mrefu.

"Mafanikio mengine ni kwamba hivi sasa tunajua mwezi Agosti na Septemba ni kiasi gani cha mafuta kinatarajiwa kuingia nchini, lakini zamani haikuwa hivyo, kwani ulikuwa huwezi kujua kiasi cha mafuta yanayotarajiwa kuingia nchini mpaka siku yatakapofika," anasema.

Mulokozi anajivunia mafanikio mengine ni kuanzishwa sehemu zingine za kupokea mafuta bandarini, kutoka moja iliyokuwapo kabla ya mwaka 2015. Hapo anataja fursa mpya za Bandari za Tanga na Mtwara, kutoka Dar es Salaam pekee wakati huo.


Ni aina ya ushindi kwa mujibu wa Mulokozi, kwani nchi jirani za Zambia, Malawi, DRC, Rwanda na Burundi zimefurahishwa na mfumo huo na zinapitisha mafuta yake Tanzania.


"Zamani asilimia 20 mpaka 30 ya mafuta tuliyokuwa tukiagiza yalikuwa ya nje ya nchi (on transit cargo), lakini kwa sasa yanayopita nchini yanafikia hadi asilimia 49 wakati asilimia 55 ni ya matumizi ya hapa nchini," anahitimisha Mulokozi.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Ubaguzi, matusi havituachi salama



NA JOSEPH KULANGWA

MEI 25 mwaka huu ni siku itakayokumbukwa daima duniani kote. Wataikumbuka wazungu na Waafrika, weupe kwa weusi. Ndiyo siku aliyouawa kikatili Mmarekani mwenye asili ya Afrika, George Floyd.

Floyd aliuawa kwa kuminywa shingo lake kwa goti la askari polisi mweupe, Dereck Chauvin wa Minnepolis, Minnesota, Marekani, kwa sababu zisizo na mashiko hata kidogo.

Chauvin na askari wenzake watatu wako nyuma ya nondo, wakisubiri hatima yao. Sababu zisizo na mashiko tu!

Kwamba siku hiyo ya Jumatatu, Floyd alienda katika duka moja hivi mtaani kununua sigara. Akatoa noti ya dola 20. Muuza duka akang'aka kuwa dola ile ilikuwa bandia hivyo akamwitia polisi.

Kwa kuwa alikuwa na uhakika kuwa noti yake ni halali (ikathibitika kuwa halali) wala hakuhamanika, akasubiri kuona nini itafuata, kwani hata alipojitetea kuwa noti ile haina matatizo, polisi walifika na kumdaka. Alijitetea akikataa kukamatwa.

Lakini, kwa kutumia nguvu za ziada aliwekwa chini na kufungwa pingu za mikono mgongoni na Chauvin akampigia goti la shingo kwa dakika 8.46 hivi, hata alipolia kwa uchungu kuwa anashindwa kupumua, polisi huyo jasiri hakujali, akaendelea kumminya hapo chini.

Akapoteza maisha kizembe mwananchi huyo, tena mbele ya macho ya askari wengine na baadhi ya raia waliokuwa wakishuhudia pamoja na msichana mweusi aliyerekodi tukio lile kwa simu yake ya mkononi na kuisambaza duniani kote, kwenye mitandao ya kijamii.

Baada ya video hiyo kuonekana, kama mlivyojionea wenye akili timamu na macho mangaavu, hakuna tena aliyejali karantini ya Kovidi au mama yake, watu waliingia barabarani kupinga walichokiona.

Si Marekani, si Ulaya, si Asia, siAfrika, si Mashariki ya Mbali, hakuna sehemu ambako maandamano hayakufanyika.

Watu waliingia mitaani na barakoa zao kuhanikiza dhidi ya walichokishuhudia. Ingawa sicho hasa.

Sicho hasa. Watu walifukua makaburi. Watu waliona hapo sasa ndipo pa kuanzia. Weusi wengi walishauawa kibaguzi, situ Marekani bali hata Uingereza na kwingineko. Afrika Kusini haikusazwa.

Mauaji yalitokana na ubaguzi, ubaguzi wa rangi. Siku hiyo wakaona basi tutokee hapa, kwa sababu imetosha. Tumeuawa sana, tumebaguliwa sana. Inatosha sasa tunataka mabadiliko, tunataka kuheshimiwa, tunataka kutambuliwa.

Floyd akawa ameifunua dunia, ameuambia ulimwengu na kama mtu aliyejitoa mhanga kuwakomboa wenzake. Mambo hayajatulia.

Tukio la Floyd lilinirudisha kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 toleo la 2005, nikajikita kwenye Sehemu ya Tatu, Ibara ya 12 (5) inayosema: "...neno kubagua maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabila, pahala walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali yao ya maisha, kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi, ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima..."

Katiba iko wazi sana hapa. Je, tunaielewa na kuitekeleza? Tunaiheshimu? Nahoji hivi nikijua kimbembe cha Oktoba kimeanza, watiania wameshatia, fomu zimechukuliwa, wadhamini wanatafutwa na hatimaye, Inshallah, Oktoba mambo yatakuwa mambo.

Tubaguane kama alivyofanyiwa Floyd na mamilioni kwa mabilioni ya watu duniani? Mhaahwapi! Najua tutasikia mengi majukwaani na kwingineko katika kinyang'anyiro hiki!

Pamoja na kwamba Rais John Magufuli ameshahadharisha na kuwasihi watu wasitukanane, najua hakuna anayeruhusu matusi, lakini Watanzania tunajuana. Tuwakemee.

Hata kabla ya uchaguzi tu, watu tumeanza kubaguana kiitikadi na kuitana majina ya matusi matusi, itakuwaje kwenye kinyang'anyiro? Anaibuka mtu anasema eti hawa ni wa chama cha... Mwingine anasema hawa ni sawa na... Kweli? Huu si ubaguzi kweli?

Watu walewale, binadamu walewale walioumbwa na Mungu yule yule kwa mfano wake, mnatukanana, kweli si kumtukana Mungu wenu kweli? Kisa kura! Acheni hizo. Ubaguzi hautatuacha salama. Tutakuwa tunakula nyama ya mtu na tutaangamia. Alamsiki.

**• Simu: +255 713 410008 na barua pepe:jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

# Corona umeziweka njia panda miradi majengo marefu ‘majuu’

- Ujenzi maghorofa umesimama kusikilizia
- Mengi mapya; ufanyaji kazi, mahitaji yake
- Soko la Hisa nalo ladondokea ulingo mpya

**Na Nimi Mweta**

WAKATI bado hali ni ngumu katika mapambano dhidi ya virusi vya corona barani Ulaya, Marekani na kwingineko, athari za kiuchumi za watu kufanya kazi za ofisi wakiwa majumbani zinachukua sura tofauti.

Kuna namna hali hiyo inaanza kuzoeleka, huku uwezekano wa watu kuondokana na maambukizi ya corona hauonekani katika maeneo mengi.

Wimbi la corona iliyopita, kama ilivyo nchini Tanzania, haiko katika nchi nyingi duniani, ila kwa jumla Afrika hadi sasa ina afueni kubwa dhidi ya maambukizi yake.

Moja ya maeneo yanayoleta utata kimkakati, ni namna ya uendeshaji biashara kama utarudi katika namna ya zamani, baada ya watu kufaulu kujiendesha wakiwa majumbanii.

Kuna utafiti kadhaa zenye ripoti kuwa, watu wanapofanya kazi kutoka nyumbani na kwa sehemu kubwa wafanyakazi walio wataalamu, wanafurahia mfumo mpya walio nao kati ya maisha na kazi katika zama zilizopo za janga la corona.

Ni kwamba hawana haraka au shauku ya kuanza tena kuamka mapema hata alfajiri, katika kujiandaa kwenda ofisini. Ni hali inayoleta sura mpya katika uwekezaji wa ardhi, ambako ujenzi wa majengo marefu ya ofisi utapungua.

Hata hivyo, bado ni hali isiyoweza kuthibitishwa kwamba ama itadumu au la. Jambo kuu ni kwamba, inaelekea kukubalika kutoka kampuni kubwa na hasa nchini kama Marekani, ambako kumemezwa sana na janga corona.

Kwa ujumla kunaonyeshwa njia katika masuala ya uwekezaji na mitaji inakoelekea. Ina maana, kasi ya ujenzi wa majengo marefu ya ofisi ambayo ni sekta muhimu katika miji mikubwa, kila mahali sasa inaanza kuchukua sura mpya.

Hapo ni pale waajiri watagundua kuna faida za kuwezesha watu wafanye kazi kutoka majumbani mwao na kuna ubashiri wa kuonekana uwezekano wa kukaa majumbani kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza tija, kupunguza gharama na hata viwango vya mishahara kwa wajiriwa.

**MAGEUZI YALIVYO**

Kwa wastani wa muda fulani, zuio la kutofanya shughuli za kawaida na kufungwa huduma nyingi za kijamii kumedumaza sekta ya nyumba na ardhi kwa jumla.



Ujenzi unapendelea huko, Pennsylvania, Marekani. Picha ya chini, majengo ya jijini Chicago. Hivi sasa janga la corona limeweka njia panda soko la majengo yaliyokamilika na yanayoendelea kujengwa, yamesitishwa kusikilizia hatima ya corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Ziko dalili kuwa utandawazi uliopo katika sekta ya ardhi na nyumba, utashika kasi zaidi kuvutia wawekezaji kutoka nje na tayari nchi kadhaa za Ulaya zimeshachukua hatua kuondoa kodi za ununuzi au ubadilishaji miliki za makazi.**



Hiyo ni kwa sababu, siyo rahisi kwa wakala kuonyesha watu maeneo ambayo yako wazi, au yanauzwa. Pia, biashara za kila sekta zinaingia shakani kutokana na wimbi la maambukizi na zuio la kutotembea.

Mengine hapo yanahusu kufungwa kwa huduma na kupunguzwa kazi idadi kubwa ya watu, mipango mingi ya ofisi kuhama katika mtazamo wa kupata eneo zuri zaidi la kufanyia kazi, iliwekwa kapuni.

Wataalamu wanasema kwamba, ikilinganishwa na mtikisiko wa fedha na mabenki wa mwaka 2007/2008, mwaka huu kuna afueni kwani nyenzo za biashara kusimamia zilishabadilika.

Kuna mabadiliko ya kiteknolojia, kwa kuwapo sekta zilizofanya vizuri wakati wa zuio la kutotoka majumbani kuwepa au kutokutana watu wengi wa eneo moja, hasa zile zinazotoa huduma kwa mtandao ‘kumbakumba’ ya corona.

Ufanyaji kazi majumbani uliongeza hitaji la vifaa kama kompyuta na vinginevyo, ambavyo kwa kawaida siyo lazima kila mmoja kuwa navyo katika makazi yake.

Watu katika hatua hiyo mpya, wanalazimika kununua vifaa bora zaidi vinavyohimili ufanyaji kazi na hakuna msaada jirani wa kiofisi, unaopatikana kwa haraka mahali hapo nyumbani.

Ni hali inayomfanya mtendaji anaangukia mbadala kama kumtumia fundi wa kujitegemea mtaani.

Pia, kuna maeneo ya huduma za kukidi mahitaji kma mlo, kwa wakati huo mtumishi hana haja nayo, kwani yupo anafanya kazi zake katika chumba binafsi cha maskani aliyo nayo, akipata urahisi wa kujipanga baadaye afurahie burudani zake, iwe muziki au dansi.

**SOKO LA HISA**

Watafiti soko la mitaji na hisa nchini Marekani, wanasema kukwama kuendelea kwa majengo ya kibiashara na hata makazi ya watu, ni zao la kinachojengwa kampuni kubwa, daima si watu binafsi.

Soko hilo limepamba moto hivi sasa, kwani mahitaji ni makubwa zaidi ya nafasi au makazi yaliyopo wazi na kuna punguzo la viwango vya riba katika benki za biashara, ambako kumesaidia kuongeza idadi ya wanaomudu kununua nyumba, makazi au kutanguliza fedha zinazostahili kuingia mkataba wa ununuzi.

Inaelekea kuwapo uwezekano wa kufanya kazi majumbani kutaongeza hitaji la makazi yenye nafasi zaidi na hata nyumba za kifahari, kwani suala la kujiburudisha kwa kutoka nje au kuogelea, itakuwa ni la kujipangia muda.

Ziko dalili kuwa utandawazi uliopo katika sekta ya ardhi na nyumba, utashika kasi zaidi kuvutia wawekezaji kutoka nje na tayari nchi kadhaa za Ulaya zimeshachukua hatua kuondoa kodi za ununuzi au ubadilishaji miliki za makazi.

Upande mwingine, kunatajwa matarajio ya kupanuka sekta hiyo kunaendana na ongezeko la mitaji, kwa sababu fedha sasa zinahamishwa kutoka nchi zinazoendelea kutafuta faida katika hisa na sekta ya makazi ndani ya nchi tajiri.

Hiyo imefikia kiasi kwamba, baadhi ya wataalamu wanatazamia katika miezi mitatu ya mwisho ya mwaka huu, yaani kuanzia Oktoba itakuwa inarudia hali ya kawaida, ingawa inategemewa kuwa mapema kuhibitisha uhakika wa kuchukua sura hiyo.

Kuna mchambuzi anayeeleza kuwa, sekta ya makazi katika nchi hizo zilizotajwa zitazinduka kwa hatua, huku picha halisi ya kupatikana nafasi za ofisi, zitategemea kati ya mwekezaji wa kampuni moja na nyingine; mji au jiji moja hadi jingine, na hapatakuwapo kanuni za jumla.

Swali kuu linalojitokeza ni kwamba, kupungua kwa kiasi kikubwa uhitaji wa nafasi za ofisi, unayaweka njia panda majengo marefu katika maeneo mengi duniani ambayo ujenzi wake sasa umesimamishwa.

Kikuu hapo ni ubashiri wa sintofahamu ya kufumuka corona dhidi ya uchumi na kama yatamalizika, basi majengo hayo makubwa yatumike kama ofisi, au yageuzwe kuwa maskani ya kupangisha.



# Kigogo CHADEMA auawa kwa mshale

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MWENYEKITI wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Palanga wilayani Chemba mkoani Dodoma, Asia Saidi, ameuawa kwa kuchomwa mshale.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, chanzo cha kifo hicho ni mgogoro wa wakulima na wafugaji.

"Ni kweli aliuawa na mtu aliyewavizia usiku na kumchoma mshale wa sumu na alikufa wakati akikimbizwa Hospitali ya Kondoa kwa matibabu, muuaji amekamatwa lakini chanzo siyo siasa, bali kulikuwa na ugomvi wa wakulima na wafugaji, taarifa kamili tutazitoa," alisema Odunga.

Alidai kuwa chanzo cha ugomvi huo ni ng'ombe wa marehemu kuingia kwenye shamba la alizeti la mtuhumiwa wa mauaji hayo na kusababisha mzozo kati ya pande hizo mbili.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kati, Mbughi Gwamaka, pia alidai jana kuwa kifo hicho hakihusiana na mambo ya kisiasa kutokana na taarifa za eneo la tukio.

Awali, zilisambaa taarifa kutoka eneo la tukio zikidai kuwa, Asia alipigwa mshale wa sumu wakati akitoka kwenye mkutano wa kura za ndani za chama hicho kwa ajili ya kumpata mgombea ubunge.




Malori yakishusha mizigo eneo la Barafu nje ya Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, jana. Jiji hilo lilikuwa na uhaba wa maeneo rasmi ya maegesho ya malori ya mizigo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Simbachawene: Polisi wajipange uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

JESHI la Polisi nchini, limepunguza matukio ya uhalifu na kuziba mianya ya uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya, usafirishaji wa binadamu na uhalifu unaovuka mipaka.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliyasema hayo katika kikao kazi cha Maofisa Wakuu Makao Makuu, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na vikosi kinachofanyika jijini hapa kwa siku tatu kwa lengo la kufanya tathmini ya utendaji wa kazi za jeshi hilo.

"Tumefanikiwa katika maeneo fulani kwa kiasi hiki, tuseme kwa nguvu Watanzania wasikie, majirani zetu wasikie na dunia nzima, mafanikio haya ni makubwa sana.

"Kama tusiposema, wale wakutusema mabaya. Watazidi kusema wao yale mazuri tuliyoyafanya hayatajulikana. Kwa hiyo, tusibweke, tuendelee kujipanga zaidi kuhakikisha kiwango cha uhalifu nchini kinatokomezwa," alisema.

Alilitaka jeshi hilo kujipanga zaidi kiteknolojia kwa kuwa mfumo wa uhalifu duniani umechukua sura mpya kwa kukua teknolojia ya mawasiliano.

"Kumekuwa na matukio ya ugaidi, utengenezaji na usambazaji wa bidhaa bandia, makosa ya kimtandao, wizi wa magari, utoroshaji madini kwa magendo, ujangili pamoja na makosa mengine yanayoambatana na hayo," alisema.

Kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, waziri huyo alisema jeshi hilo lina wajibu wa kuhakikisha unakuwa huru na haki.

"Kazi mnayofanya ni kubwa na nzuri kuhakikisha mwananchi na mali zake anakuwa katika hali ya usalama, lakini sasa mchakato wa kupata wagombea unaendelea nchi nzima.

"Tunaenda kwenye uchaguzi, tunapaswa kujipanga vizuri kupambana na vitendo vyovyote ama viashiria vya uvunjifu wa amani nchini kwetu," aliagiza.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, alisema vyombo vya ulinzi na usalama vimejipanga kuhakikisha hali ya usalama hususani wakati wa uchaguzi huo inakuwa imara na kuwataka wananchi na wanasiasa kutimiza wajibu wao kwa kutojiingiza kwenye vitendo vya uvunjifu wa amani.

# Machinga waomba wapewe mikopo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA wanaojishughulisha na biashara ndogo mkoani Dodoma, wameiomba serikali kuwapatia mikopo ili kuongeza mitaji ya biashara zao.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Soko la Sabasaba jijini hapa, Emmanuel Mtega, aliwasilisha kilio cha vijana hao wakati wa uzinduzi wa umoja huo.

Alisema vijana wengi nchini wanajishughulisha na biashara ndogo, lakini wanakabiliwa na tatizo la kutokuwa na mitaji.

Kiongozi huyo alisema kwa sasa wamejiunga ili kupata fursa ya mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha ikiwamo ya ile ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

"Tunajua kuwa mtu mmoja mmoja hawezi kwenda benki kukopa fedha, lakini tukiwa na kikundi au kwenye umoja, tunaweza kupata fursa hiyo kuanzia kwenye mikopo ya halmashauri hadi kwenye benki kwa kuwa umoja wetu unatambulika," alisema.

Mtenga aliongeza kuwa lengo la umoja huo mbali na kuwa na uhakika wa mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na halmashauri, ni kuhakikisha wanakuwa na Chama cha Akiba na Mikopo (Saccos) ambacho wafanyabiashara watakuwa wanakopa fedha kwa ajili ya kuendesha biashara zao.

Alisema umoja huo umewakusanya vijana wote ambao ni wafanyabiashara kwenye eneo hilo ili kuwainua kwenye biashara zao kwa kuwa wengi wao ni wale wanaojishughulisha na biashara ndogo ndani ya Soko la Sabasaba.

"Lengo kuu la kuanzishwa kwa umoja huo ni kuwawezesha vijana kujiongezea kipato na kuweza kusaidia familia zao kwa kuwapa mitaji au kwa kuanza na mtaji mdogo hadi kufikia mtaji mkubwa," alisema.

Katibu wa Umoja huo, Dickson Msungu, aliwataka vijana kujitokeza na kujiunga ili kufanya biashara zao kwa pamoja badala ya kukaa mitaani na kuilalamikia serikali kuwa haitoi ajira.

Alisema Tanzania imeshaingia kwenye uchumi wa kati, hivyo ni jukumu la kila kijana kuhakikisha kuwa anaendana na kasi hiyo ili kuinua zaidi uchumi wa nchi.

Mmoja wa wanachama, Hilda Ngoye, alisema kuwa umoja huo ulianzishwa mwaka 2019 na mpaka sasa una jumla ya wanachama 105 ambao kila wiki wanatoa ada ya Sh. 3,000,





# Mgombea udiwani viti maalum CHADEMA apeta

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MGOMBEA udiwani viti maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Vumilia Anderson, ameibuka kidedea baada ya kupata kura 21 kati ya 131 zilizopigwa na wajumbe wa Baraza la Wanawake wa Chama hicho (BAWACHA) katika Jimbo la Mbeya Mjini.

Uchaguzi huo ulifanyika jana jijini Mbeya katika eneo la Soweto kwa wajumbe wa mkutano mkuu kupiga kura za maoni kwa ajili ya kuwachagua wawakilishi wa madiwani viti maalum kutoka kata 36 za jiji hilo.

Mshindi wa pili alikuwa ni Tausi Kasege, ambaye alipata kura 16 huku washindi wa tatu wakigongana, Halima Kayeta na Joyce Mwalalika wote wakipata kura tisa. Msimamizi wa uchaguzi huo, Lucy Ngondo, ambaye ni Katibu wa BAWACHA Mkoa wa Mbeya, aliwataka watiania ambao kura zao hazijatosha kuonyesha ushirikiano na kwa wale ambao watapata ridhaa ya kuwa madiwani viti maalum.

Ngondo alisema uchaguzi huo ulikuwa huru na haki na kwamba kinachosubiriwa kwa sasa ni kamati kuu kufanya uamuzi kwa watiania wote wa nafasi ya udiwani viti maalum.

"Zoezi bado linaendelea huu sio mwisho, nawaomba wajumbe muwe wavumilivu, mchakato bado unaendelea kamati kuu itakaa na kuwachagua wanaofaa hivyo haki itatendeka," alisema Ngondo. Mmoja wa watiania ambaye kura hazikutosha, Amina Msula (81), alisema licha ya umri alionao, alitiania ya udiwani viti maalum lengo likiwa ni kuwasaidia wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wapate chakula wawapo shuleni.

Alidai licha ya kura kutokutosha alisema ataendelea kushirikiana na washindi ili kutimiza azma ya kuwatumikia wananchi wa Jiji la Mbeya kwa kuwaletea maendeleo.



Mtiania udiwani viti maalum wa Kata ya Isanga katika Jiji la Mbeya kwa tiketi ya Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Amina Msula (81), akiomba kura kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho, wakati wa kura za maoni jijini humo jana. Alipata kura moja kati ya 131 zilizopigwa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Polisi yakamata tisa kwa tuhuma za uhalifu

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeendelea na operesheni kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo na jumla ya watuhumiwa tisa kwa kipindi cha wiki moja wamekamatwa kwa makosa mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Sebastian Mbuta, miongoni mwa waliokamatwa katika operesheni hiyo ni Justine Sadiq (18), fundi rangi na mkazi wa Ndola katika mji mdogo Mbalizi akiwa na mali mbalimbali za wizi ikiwamo televisheni, deki, rimoti na tarakishi mpakato moja.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa Julai 20, majira saa 11 alasiri katika Kijiji cha Mwapalala, Kata ya Iwindi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Katika hatua nyingine jeshi hilo linawashikilia watu wawili Maulid Ngole (37) na Fred Mtega (36), wote wakazi wa Uyole kwa tuhuma za kupatikana na unga udhaniwao kuwa ni dawa za kulevya aina ya heroine gramu 10.

Watuhumiwa hao walikamatwa Julai 21 majira ya saa nane eneo la Uyole baada ya kufanya upekuzi na kukuta unga unaodhaniwa kuwa dawa za kulevya kete mbili za heroine.

Kufuatia matukio hayo, Mbuta alitoa wito kwa jamii kuacha matumizi ya dawa za kulevya kwa kuwa ni hatari kwa afya zao.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kuacha kujihusisha na biashara haramu ya vipodozi vyenye viambata vya sumu pamoja na wananchi kuwa makini kipindi wanapofanya usajili wa laini zao za simu, ili kuepuka kadi zao kutumika kusajili watu wengine.

# Wafanyabiashara ndogo walalamika kutozwa kodi

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

WAFANYABIASHARA ndogo za mboga na matunda katika soko la Lembuka, Kiwira wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wamelalamika kuwa licha ya kununua vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais Dk. John Magufuli, bado wilaya hiyo, inaendelea kuwatoza kodi.

Waliyasema hayo jana wakati wakizungumza na Nipashe na kudai licha ya kuwa na vitambulisho kama agizo la Rais Dk. John Magufuli, bado wanaendelea kutozwa ushuru wa mazao usiozidi tani moja.

Jacob Mwakandwike ambaye ni mfanyabiashara mdogo sokoni hapo alisema, licha ya kununua vitambulisho vya ujasiriamali bado wanaendelea kutozwa ushuru kama ilivyokuwa kabla ya kuvinunua. Alisema kutokana na hali hiyo hawaoni umuhimu wa vitambulisho hivyo kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inaendelea kuwatoza ushuru kinyume na maelekezo waliyopewa kabla ya kununua vitambulisho hivyo.

"Tuliambiwa tukinunua vitambulisho vya ujasiriamali hatutaendelea kutozwa ushuru, lakini hali ni tofauti kabisa kwenye soko hili, halmashauri inaendelea kutoza ushuru kama kawaida na hata hatuoni umuhimu wa kuvinunua," alisema Mwakandwile.

Kwa upande wake, Lugano Mwaipopo, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe pia inatoza ushuru wa mazao hata kwa watu wanaosafirisha chini ya tani moja kinyume cha maelekezo ya Rais Magufuli ambayo wamekuwa wakiyasikia kwenye vyombo vya habari.


"Tunashangaa hata ukija na gunia moja la mazao kama vile mahindi, vitunguu au kabeji wanakulazimisha ulipe ushuru, lakini tulimsikia Rais akizungumza kwenye vyombo vya habari anasema ukiwa na mazao chini ya tani moja hupaswi kulipa ushuru," alisema Mwaipopo.

Mwenyekiti wa soko hilo, Juma Asante, alisema baada ya kupokea malalamiko ya wafanyabiashara hao wadogo, aliiandikia barua Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuomba wasitishe ushuru huo ili kuondoa kero kwa wafanyabiashara wadogo, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

"Nilishaiandikia barua zaidi ya nne Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuhusu malalamiko haya, lakini wanapuuza na kuendelea kutoza ushuru huu unaolalamikiwa, sasa tunaomba habari hizi zimfikie Rais ili awasaidie wajasiriamali hawa," alisema Asante.

Akikabidhi vitambulisho vya wajasiriamali kwa wakuu wa wilaya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kila mfanyabiashara mdogo atakayenunua kitambulisho cha ujasiriamali hapaswi kutozwa kodi yoyote inayohusiana na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA).

Hata hivyo, alisema kitambulisho hicho cha ujasiriamali, hakimwepushi mhusika kulipa ushuru wa mazao waliokubaliana kwa ajili ya huduma zao wenyewe kama vile kulipia umeme, usafi na utunzaji wa mazingira.





# DC ataka bajeti mabaraza ya wazee

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaskazini B Unguja, imetakiwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya mabaraza ya wazee wa shehia 31 za wilaya hiyo, ili wanufaike na fedha zinazokusanywa ndani ya halmashauri hiyo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rajab Ali Rajab, alisema hayo jana kwenye ukumbi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mahonda wakati akizindua mabaraza ya shehia ya wilaya hizo.

Alisema wazee wamefanya shughuli nyingi ikiwamo ya kulinda amani na utulivu uliopo, hivyo ipo haja ya kuendelea kuwatunza, kuwaenzi na kuwapatia huduma muhimu za jamii ikiwamo afya.

Rajab aliitaka halmashauri hiyo kutoa kipaumbele kwa wazee pale wanapofika katika vituo vya afya kupata huduma za matibabu.

"Kwenye huduma za jamii zote lazima tuwape kipaumbele wazee kwanza kuliko vijana vinginevyo sitamvumilia ofisa yeyote atakayemwacha mzee kukaa foleni anapofika kwenye vituo vya afya kupata matibabu," alisema.

Mkuu wa wilaya alisema kuwapo kwa mabaraza ya wazee kutarahisisha upatikanaji wa huduma kwa kundi hilo pale watakapohitaji huduma na wataweza kupeleka malalamiko yao kwenye mabaraza hayo.

Aliwataka wazee kupanga mipango yao na kupeleka katika halmashauri ili yafanyiwa kazi na kutumia nafasi hiyo kuahidi kuwa wilaya yake itasimamia haki za wazee ikiwamo kupatiwa pensheni kwani ni haki yao.

"Tunamshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kutoa pensheni kwa wazee na kwa hili nitahakikisha kila mzee aliyefikia umri wa hupatiwa haki hiyo ninasimamia," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Rajab, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, alisema watajenga ofisi ya baraza la wazee na kupata sehemu ya kuendesha shughuli zao na mabaraza hayo kukutana kufanya majukumu yao.

Aliwataka wazee kuwashirikisha wazee katika mabaraza hayo na wao watoe michango yao.

Mkuu huyo alimpongeza Rais Dk. Shein kwa kutia saini sheria inayowahusu wazee ambayo itaimarisha ustawi wa wao kwa maslahi ya maisha yao.

Naye Mratibu wa Miradi wa Jumuiya ya Wazee (JUWAZA), Halima Omar, aliipongeza wilaya hiyo kwa uamuzi wa kufanya uzinduzi wa mabaraza hayo ili kuwezesha wazee wapate stahiki zao.

Kwa upande wao wazee, walisema watashirikiana katika kuendesha mabaraza hayo ili kila mzee apate haki yake katika mabaraza.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (katikati), akikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa hoteli ya kimataifa ya Golden Tulip, iliyopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Polisi yakoleza operesheni dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja limesema litaendelea kufanya operesheni za kupambana na watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya mkoani humo. Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa huo, Haji Abdalla Haji, alisema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari kutokana na kukamatwa kwa dawa za kulevya kwa kijana Suleiman Omar Suleiman (30), mkazi wa Nungwi Wilaya ya Kaskazini A, Unguja.

Kamanda Haji alisema tukio hilo lilitokea Julai 21, mwaka huu, majira ya saa 4:30 asubuhi. Mtuhumiwa huyo alipatikana na kete 81 za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa gramu 1.782.

Kamanda Haji alisema kete hizo zilipatikana zikiwa zimefungwa ndani ya paketi ya sigara na kuhifadhiwa ndani ya suruali fupi ya mtuhumiwa aliyokuwa ameivaa ndani. Alisema jeshi hilo likiwa katika operesheni ya kupambana na watumiaji, wasambazaji na wauzaji wa dawa za kulevya, lilimkamata mtuhumiwa huyo na kusema atapelekwa mahakamani mara taratibu zitakapokamilika.

Haji aliwataka vijana kuacha kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya kwa kuwa wanaangamiza nguvu kazi ya taifa badala yake watafute shughuli halali wafanye.

# Waanika dagaa waomba msaada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Waanika Dagaa wa eneo la Mangapwani, Mohammed Omar Makame, ameiomba serikali kuwasaidia kuwatatulia changamoto zinazowakabili ikiwamo ya kuwajengea sehemu ya kuhifadhia mizigo yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema kutatuliwa kwa changamoto hizo kutawasaidia kupata sehemu ya uhakika wa kuanika pamoja na kupata sehemu ya uhakika ya kuhifadhi mizigo yao.

Pia alisema katika eneo hilo wanakabiliwa na tatizo la majisafi na salama na uchache wa vyoo vya kudumu, jambo ambalo linahatarisha usalama wa afya zao.

"Tatizo hili tumeshalipeleka ofisi za halmashauri ya wilaya hadi mkoa, lakini bado limekuwa likiendelea. Tunaomba kusaidiwa ili tufanye kazi zetu kwa amani zaidi," alisema.

Mwenyekiti huyo aliomba serikali kuangaliwa upya bei elekezi ya dagaa kama iliyowekewa katika zao la mwani na kuwashauri wapishi wa dagaa kuweka mfumo wa kutumia majiko ya gesi ili kuhifadhi mazingira.

"Miti imekuwa ikihujumiwa sana hivi kutumia nishati ya gesi itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira ya ukataji wa miti ovyo," alisema.

Naye Subira Faki Kombo, mfanyabiashara wa kuanika dagaa, alisema kuwapo kwa ghala la kuhifadhia mizigo kutawanufaisha waanika dagaa kuondokana na tatizo la wizi wa vitu vyao wanavyofanyia kazi.

Aliomba serikali kuliangalia suala hilo na kwamba kazi hiyo inawasaidia kukidhi mahitaji ya familia zao na wengine wamekuwa na hali ngumu na ni wajane.

Pamoja na hayo, aliomba serikali kuwapatia mikopo isiyo na riba ili kuwasaidia kujinyanyua zaidi kimaisha kwa kufanya biashara itayoweza kuwanyanyua zaidi na kujiendeleza kimaisha bila ya kuhitaji msaada.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDITH SERAFINI LUCINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 819 CVR Mitsubishi Canter. Chassis namba FE317BD443564.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Control No: 9910818043123.**

158229

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 80 YA 2020**
**BAINA YA**
**VIOLET BIGAMBO MAFURU……………MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1. JOYCE WILSON RUVYAGILA**
**2. DAVID DANIEL SENDEU……………………WADAIWA**

KWA: JOYCE WILSON RUVYAGILA - POPOTE ULIPO

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 07.09.2020 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO: Kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 ya Mwezi wa Julai, 2020.

R.S.K. Mandari,
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

158227

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NO. 39 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ABDULSHAKUR ABDALLAH GULMOHAMED – DECEASED**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**SABRINA ABDULSHAKUR ABDALLAH**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 Mwezi wa 8, 2020.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10 Mwezi wa 7, 2020.

NAIBU MSAJILI

NAKALA KWA:
Innocent Tairo Adv
Tairo Law Office (Adv)
1st Floor ... Build
Apartment No 101 & 102
D' Salaam

158183

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 192/2020**

Ombi la OMARY ATHUMANI MKUYU,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AYUBU ATHUMANI MKUYU. Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/07/2020.

158183

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA UTEKELEZAJI WA MADAI KIKAZI NA 27 YA 2019**
**FLORENCE FELICIAN……………….MDAI**
**DHIDI**
1. KING'S INSURANCE BROKERS LTD………MDAIWA
2. TRICO INSURANCE BROKERS LTD ……….MDAIWA
Kwa 1. KING'S INSURANCE BROKERS LIMITED
2. TRICO INSURANCE BROKERS LIMITED

**KUITWA SHAURINI**

Fahamu kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo ninyi ni wadaiwa limepangwa kusikilizwa mbele ya mahakama hii tarehe 10.08.2020 saa 3:00 asubuhi.

Hivyo mnatakiwa kuhudhuria mahakamani nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu siku hiyo bila kukosa.

Kutokuhudhuria kwenu kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila nyinyi kuwepo.

Imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 25 mwezi juni, 2020

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA.

158234

### KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**MSAFIRI OMARY HASSANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 553 ADY T/CRUSER. Chassis namba HZJ750045814. Engine namba 1HZ0255750. Kadi ya gari yenye namba za usajili T 863 DDG aina ya T/SPARKY. Chassis namba 522IE0003164. Engine namba K3VET.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/KIJ/RB/548525/2020.

158229

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BARAKA ISAAC CHALLE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 802 CJS TOYOTA HARRIER. Chassis namba MCU100038242. Engine namba 1MZ4350980.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/KIJ/RB/183986/2020.

158229

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

**Nipashe**
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-20 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,427 | 3,522 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,683 | 11,307 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33,857 | 33,333 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,390 | 2,922 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (58) | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 100,334 | 102,996 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 127,070 | 126,880 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 32,616 | 32,390 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,480 | 3,583 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **311,799** | **317,933** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 100,654 | 97,144 |
| 18 | Amana za Wateja | 93,439 | 100,589 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 28 | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,737 | 6,150 |
| 28 | Madeni | 72,301 | 71,060 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **269,159** | **274,943** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **42,640** | **42,990** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,065 | 1,065 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (81,099) | (80,526) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (983) | - 633 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 704 | 130 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,640** | **42,990** |
| | | (0) | - |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 3,207 | 3,493 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 24,477 | 19,691 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,171 | 15,750 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13.68% | 13.52% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 17.05% | 13.81% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74.32% | 72.13% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40.75% | 39.91% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.20% | 83.71% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.84% | 3.17% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.93% | 2.83% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,642 | 10,765 | 20,887 | 21,187 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,678) | (4,679) | (9,429) | (9,453) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,964** | **6,086** | **11,458** | **11,734** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 259 | 534 | 859 | 1,096 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (106) | (719) | (524) | (1,454) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **844** | **1,324** | **1,916** | **2,617** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 223 | 532 | 703 | 999 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 169 | 713 | 350 | 1,377 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 451 | 79 | 864 | 241 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,277)** | **(8,014)** | **(14,625)** | **(15,992)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,486) | (2,792) | (5,021) | (5,327) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,792) | (5,222) | (9,604) | (10,665) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(316)** | **(790)** | **(915)** | **(1,999)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (34) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(350)** | **(835)** | **(983)** | **(2,090)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(350)** | **(835)** | **(983)** | **(2,090)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 151 | 160 | 151 | 160 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.14) | (0.34) | (0.10) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 7 | 6 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.22% | -0.53% | -0.62% | -1.32% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -1.63% | -3.12% | -4.59% | -7.80% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 106.89% | 108.15% | 109.35% | 111.43% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.82% | 1.76% | 3.49% | 3.39% |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 24-Jul-20 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 24-Jul-20 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 24-Jul-20 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 24-Jul-20 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 24-Jul-20 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-20 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (316) | (599) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,426 | 1,834 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (191) | 876 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (10) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (3,773) | 6,071 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - 524 | (281) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3,236) | 3,301 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (226) | (5,842) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (34) | (34) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(6,883)** | **5,325** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (88) | (82) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(88)** | **(82)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (6,971) | 5,242 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 120,747 | 115,504 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **113,776** | **120,747** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (983) | - | - | - | (983) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (574) | 574 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(82,082)** | **704** | **0** | **1,065** | **42,641** |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(72,910)** | **0.22** | **1,284** | **1,065** | **45,453** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8,769) | - | - | - | (8,769) |
| Hisa za upendeleo | 6,940 | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |

# MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50 000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20 000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1 500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20 000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3 000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2 000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6 000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2 000 000.00 | $ 2 000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5 000.00 | $ 10.00 | N/A |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35 000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3 000 000.00 | $ 3 000.00 | £ 3 000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100 000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1 000 000.00 | $ 1 000.00 | £ 1 000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5 000 000.00 | $ 5 000.00 | £ 5 000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500 000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25 000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10 000 000.00 | $ 10 000.00 | £ 10 000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10 000 000.00 | $ 10 000.00 | £ 10 000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25 000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |

| GENERAL CHARGES | | | |
|---|---|---|---|
| Bankers Cheque | TZS 50 000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120 000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30 000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15 000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25 000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60 000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10 000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4 000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40 000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5 000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50( | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2 500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6 000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5 000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80 000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75 000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10 000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3 000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1 000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

215823802

# HABARI MICHEZO

## PULISIC NI KAMA HAZARD CHELSEA - LAMPARD



**LONDON, England**

FRANK Lampard anaamini mchango wa Christian Pulisic kwa Chelsea unalingana na Eden Hazard wakati akicheza hapo Stamford Bridge.

Pulisic alifunga na kutoa 'asisti' wakati akitokea benchi katika kipindi cha pili wakati Chelsea ikichezea kichapo cha mabao 5-3 kutoka kwa Liverpool kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumatano usiku.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao tisa ya ligi na kutoa pasi za mwisho nne katika mechi 24, akilinganishwa na Hazard katika msimu wake wa kwanza (akifunga mabao tisa na 'asisti' 11 katika mechi 34) pale Chelsea msimu wa 2012-13.

Lampard alipaza sauti kumsifia straika huyo na alisema mchango wa Pulisic kwa Chelsea unafanana na Hazard, ambapo raia huyo wa Ubelgiji alihamia Real Madrid mwaka jana.

"Kwa hakika ni muhimu sana. Ana mchango kama wake," alisema kocha huyo mkuu wa Chelsea akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilikuwa hapa na Eden katika mwaka wake wa kwanza na haikuwa rahisi kwake kuja kwenye Ligi Kuu na kuizoea. Christian naye ana wakati mzuri sasa.

"Tangu katikati ya msimu amekuwa vizuri, tangu kuanza amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia. Ni majeruhi tu aliyopata kwenye mchezo dhidi ya Norwich yakamfanya kuwa nje kwenye nusu fainali ya kombe la FA."

## MAGUIRE: LAZIMA TUSHINDE KWA LEICESTER

**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire amekubali radhi aliyoomba Paul Pogba kwa kuisababishia Manchester United penalti kwenye mchezo wa nyumbani dhidi ya West Ham, lakini amesisitiza hakutakuwa na msamaha dhidi ya Leicester City, Jumapili.

United ilipanda kwenye nne bora katika msimamo wa Ligi Kuu ya England baada ya sare ya kufunga bao 1-1 dhidi ya wagonga nyundo hao wa London, Jumatano, ingawa walitanguliwa kufungwa kwa bao la Michail Antonio baada ya Pogba kuunawa mpira eneo la hatari.

Mason Greenwood alikisawazishia kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer na kuwahakikishia kupata pointi hiyo moja na sasa wanahitaji pointi moja tu ili kubakia kwenye nne bora, ambapo watacheza na Leicester City waliopo nafasi ya tano kwenye msimamo ili kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Pogba baada ya mchezo huo aliomba radhi kwa kusababisha penalti hiyo na nahodha wa United, Maguire alibainisha kuwa amemsamehe mshindi huyo wa kombe la Dunia na Ufaransa.

"Ilikuwa laini," alisema Maguire akiiambia Sky Sports. "Huwezi kusema ilikuwa ni kawaida kutoka kwa Paul. Angeweza kufanya hivyo? Pengine alitakiwa kukinga uso wake.

"Lakini aliomba rashi, alinyanyua mkono wake juu, wakati akijua kwamba hakutakiwa kufanya hivyo.

"Nafikiri ni jambo la kawaida katika kujilinda mwenyewe na kulinda uso wako. Sikuona vizuri - nafikiri aliulinda uso wake na mikono na akaunawa mpira.

"Sasa tupo kwenye nafasi nzuri, hivyo hakutakuwa na msamaha kwenye mchezo wetu wa mwisho dhidi ya a Leicester kwani ndio nafasi yetu ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa."



# CONTE:

## SIIFIKIRII NAFASI YA PILI

**MILAN, Italia**

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Antonio Conte amesema nafasi ya pili "ni kama ya walioteza" baada ya Nerazzurri kuachwa pointi moja nyuma ya Atalanta kwenye msimamo wa Serie A.

Kikosi cha Conte hakikuwa na makali kwenye mchezo uliomalizika kwa sare ya bila kufungana dhidi ya Fiorentina pale kwenye dimba la San Siro, Jumatano.

Romelu Lukaku na Alexis Sanchez wote waligonga mwamba kwa Inter, ambapo walikosa nafasi ya kupanda juu ya Atalanta kwenye nafasi ya pili. huku zikiwa zimesalia mechi tatu ligi kumalizika.

Inter imepitwa pointi moja na Atalanta na wakipitwa saba na vinara Juventus ambapo bingwa huyo mtetezi anakaribia kutwaa taji lake la tisa mfululizo.

"Nafasi ya pili haina maana kwa macho yangu, ni ya kwanza kwa walioshindwa," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia baada ya mchezo huo.

"Baadhi wanaona ni sawa, lakini kwa upande wangu hapana. Sitaki wachezaji wangu wafikirie kuhusu nafasi hiyo.

"Ulikuwa mchezo mzuri kwa upande wangu, tulicheza kwa mtazamo chanya kabisa na kutengeneza nafasi, lakini hatukuwa na bahati wakati tulipogonga mwamba," alisema Conte.

Nyota anayewaniwa na Barcelona, Lautaro Martinez alianzia benchi kwenye mchezo huo dhidi ya Fiorentina, huku Conte akiwaanzisha mbele Lukaku na Sanchez.

## HABARI MICHEZO

# SARRI AKUNWA UPATINA WA RONALDO, DYBALA



**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo na Paulo Dybala bado wanaweza kuimarika na kutengeneza upatina wa "kuvutia" zaidi, kwa mujibu wa kocha wa Juventus, Maurizio Sarri.

Washambuliaji hao wawili wamehusika kwa pamoja katika mabao 17 kwenye michezo 10 ya Juve tangu kuanza tena kwa ligi hiyo Juni, huku Ronaldo akicheza zaidi nafasi ya kushoto na Dybala akicheza katikati.

Ronaldo alicheza vizuri na Dybala kufunga bao la pili kwa Juve wakati wakiibuka na ushindi wa 2-1 Jumatano dhidi ya Lazio, awali akifunga la kwanza kwa penalti na kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 50 kwenye Ligi Kuu ya England, LaLiga na Serie A.

Lakini wakati Sarri akiwa anaonekana kuvutiwa zaidi na upatina wao, anaamini kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwa wawili hao.

"Inaonekana wazi kwamba wanacheza kwa ubora na kuimarisha zaidi upatina wao," alisema Sarri.

"Sioni ugumu wa kuwachezesha pamoja Ronaldo na Paulo Dybala kwani wanaonekana kuelewana zaidi wakiwa dimbani na wamefunga mabao 51 kwa ujumla wake katika misimu miwili."

# INTER YAANZA MAZUNGUMZO YA MKATABA WA MARTINEZ

**MILAN, Italia**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesema Nerazzurri hao wapo kwenye mazungumzo na nyota anayewaniwa na Barcelona, Lautaro Martinez kuhusu mkataba mpya.

Martinez amekuwa akitajwa anaondoka Inter kwenda kwa miamba wa LaLiga, Barca mwishoni mwa msimu huu, ingawa klabu hiyo ya Italia mara kwa mara imesisitiza kuwa haina mpango wa kumuuza nyota woa huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye kipengele cha kwenye mkataba wake cha kuuzwa kwa euro milioni 111 kimefikia mwisho mwanzoni mwa mwezi huu - amefunga mabao 18 msimu huu, lakini amefunga mawili tu tangu kurudi kwenye Serie A, Juni.

Marotta aliulizwa kuhusu Martinez na Alexis Sanchez anayecheza kwa mkopo hapo baada ya mchezo wa sare wa Jumatano dhidi ya Fiorentina mjini Milan.

Martinez alianzia benchi, huku Sanchez alianza na Romelu Lukaku mbele, huku Ofisa Mtendaji Mkuu huyo wa Inter, na Marotta aliiambia Sky Sport Italia: "Tumekuwa na mawasiliano na Manchester United kama tunaweza kuongeza muda wa kukaa kwa mkopo kwa Sanchez baada ya mchezo wa Ligi ya Europa na Getafe.

"Tunajadiliana kuhusu kuongeza mikataba kwa wachezaji wengi, juu ya wote vijana kwanza ambao tunataka kufanya nao kazi kwa muda mrefu, na hilo linamuhusu Lautaro.

"Tunafanya kwa utulivu, bila haraka, kwa sababu tunaheshimiana. Ana furaha kuvaa jezi yetu na atakuwa na nafasi ya kuendelea kuwa na majaliwa mazuri kwa upande wetu."




# TULIJUA TUTASHINDA MATAJI BILA RONALDO - MODRIC



**MADRID, Hispania**

LUKA Modric amesisitiza Real Madrid mara zote iliamini kwamba inatakiwa kurudi kwenye nafasi yake ya kushinda mataji baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo aliyetua Juventus mwaka 2018.

Nyota huyo wa Ureno aliondoka Madrid kwenda Turin kwa ada ya euro milioni 11 muda mfupi baada ya kushinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Los Blancos hao, alionja utamu wa taji la Serie A katika msimu wake wa kwanza nchini Italia.

Madrid walikwenda kushinda Klabu Bingwa ya Dunia mwaka 2018, lakini kwa upande mwingine walikuwa na msimu wa kukatisha tamaa, huku Barcelona wakibeba taji hilo, Liverpool ilishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Valencia wakibeba kombe la Copa del Rey.


Hata hivyo, Zinedine Zidane alirudi kuwa kocha Machi mwaka jana, na Los Blancos wakaweza kulitwaa taji la Ligi Kuu msimu huu 2019-20.

Modric amesisitiza kamwe hakukuwa na tatizo kwenye suala la morali kwa timu baada ya kuondoka kwa Ronaldo kwenda Juve.

"Huwezi kuacha kujadili kuhusu umuhimu wa Ronaldo alipokuwapo Real, lakini lazima nisema hatukuwa na mzigo wa kushindwa kubeba mataji, kwani ari yetu ilikuwa pale pale," alisema akiiambia Sportske Novosti.

"Tulishawishika kwamba tunaweza kushinda mataji hata bila yeye, kwa sababu licha ya mchango wake mkubwa kwenye timu, lakini timu ilikuwa na kila kitu cha kuweza kushinda mataji."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HENDERSON: NI HISIA TAMU KULINYANYUA KOMBE EPL

Asema ilikuwa ndoto yake tangu akiwa mtoto na ndio maana akajiunga na Liverpool ili...

**LIVERPOOL, England**

JORDAN Henderson amebainisha kwamba ni jambo la "kuvutia sana" kupata uzoefu wa kunyanyua taji la Ligi Kuu ya England, baada ya Liverpool kuifumua Chelsea 5-3 katika dimba la Anfield.

Wekundu hao walinyanyua taji la ligi hiyo Jumatano zaidi ya mwezi mmoja baada ya kushinda kombe hilo, wakiwa wamemaliza ukame wa miaka 30 kutwaa.

Hakukuwa na mashabiki ndani ya uwanja kushuhudia gwiji wa Liverpool, Kenny Dalglish akimkabidhi kombe hilo nahodha Henderson, lakini hilo halikuzuia shangwe na furaha.

Kiungo Henderson, ambaye yupo nje ya dimba kutokana na majeruhi ya goti, alisema ulikuwa wakati maalumu sana kwake kunyanyua taji hilo baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu uliopita walipoliachia kwa Manchester City.

"Kutembea tu ilinivutia. Hakika tulistahili wakati huu. Shukrani kwa familia zetu zilizokuwa zinatuangalia kupitia kwenye televisheni, kwamba hicho kilikuwa kitu kikubwa sana kwetu.

"Umekuwa msimu wa kuvutia kwa upande wetu, kulinyanyua kule ulikuwa wakati mzuri sana," alisema nyota huyo wa England akiiambia Sky Sports. "Mwanzo ulikuwa mzuri sana, na tulikuwa na msimu mzuri. Tulikuwa imara, tukijiamini zaidi, kwa hakika ulikuwa msimu wa aina yake kwa upande wetu.

"Tulipata njia ya kushinda katika maeneo mengi na tulikuwa imara na wachezaji walikuwa fiti kwa kila kitu. Wachezaji walikuwa na wakati wa kuimarisha na kuthibitisha viwango vyao."

Aliongeza: "Kupata pointi 97 mwaka jana na kutoshinda taji, lilikuwa jambo gumu kwetu kulikubali.

"Tulitengeneza nafasi chache wiki zilizofuata, sasa ni mabingwa wa ligi na halafu tutaanza tena ligi wiki chache zijazo tukiwa bado tuna kazi ya kumalizia.

"Umekuwa msimu wa kuvutia na nashukuru kuwa sehemu ya klabu hii na timu ambayo imeshinda taji la Ligi Kuu baada ya miaka 30.

"Kushinda taji la Ligi Kuu ilikuwa ndoto yangu tangu nikiwa mtoto na ndio maana nikajiunga Liverpool, nikitaka kushinda mataji na matarajio yalikuwa makubwa sana."

Liverpool itasafiri kwenda kucheza na Newcastle United kwenye mchezo wao wa mwisho wa msimu huu Jumapili wakijua kwamba wakishinda watafikisha pointi 99.

## KWA UFUPI

**ARSENAL KUMPA MKATABA MPYA AUBAMEYANG**

ARSENAL inapanga kumpa ofa ya mkataba mpya straika wake, Pierre-Emerick Aubameyang raia wa Gabon ambao utamfanya kulipwa mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki pamoja na bonasi, wakijaribu kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 abakie. ***(Telegraph)***

**NEWCASTLE YAMWANIA JOVIC**

NEWCASTLE inapanga kumchukua kwa mkopo fowadi wa Real Madrid, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 22 raia wa Serbia. ***(Shields Gazette)***

**DORTMUND MBADALA WA SANCHO**

BORUSSIA Dortmund wanamwangalia winga wa Werder Bremen, Milot Rashica mwenye umri wa miaka 24 raia wa Kosovo, kama ndio mbadala wa fowadi wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United. ***(Telegraph)***

**LEEDS YAMWANIA IBRAHIMOVIC**

LEEDS United mbayo imepanda Ligi Kuu ya England, inaweza kumsajili straika Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38 raia wa Sweden, ambaye amekubali kwamba hana uhakika wa kuongeza mkataba wake na AC Milan. ***(Sun)***

**MAN CITY KUMSAJILI BENNACER**

MANCHESTER City inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa AC Milan, Ismael Bennacer, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Paris St-Germain kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa Algeria ambaye ada yake inaweza kupanda hadi pauni milioni 45. ***(Le10 Sport)***

**WILLIAN HUYO ARSENAL**

KIUNGO wa Chelsea na Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 32, anakaribia kukubali uhamisho huru kwenda Arsenal wakati mkataba wake ukiwa unamalizika pale Blues. ***(ESPN Brasil)***

**LALLANA KURUDI SOUTHAMPTON**

KIUNGO Muingereza, Adam Lallana mwenye umri wa miaka 32, anaweza kukubali kurudi katika klabu yake ya zamani ya Southampton baada ya mkataba wake kumalizika kule Liverpool ***(Express)***

**ARSENAL YAJITOSA KWA DOUGLAS**

ARSENAL Inafikiri uhamisho wa kiungo wa Aston Villa, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 22, lakini Manchester City pia inataka kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(90min)***

**SPURS YAJIPANGA KWA PIERRE-EMILE**

TOTTENHAM Hotspur inajiamini itamsajili kiungo wa Southampton na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 24, ingawa ofa ya Everton ya pauni milioni 25 imekubaliwa. ***(Guardian)***

**GERRARD AITOSA BRISTOL CITY**

KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard amekataa nafasi ya kuwa kocha mkuu ajaye wa timu ya daraja la kwanza ya Bristol City. ***(Bristol Post)***

**VALENCIA YAWAWINDA KEPA, SILVA**

VALENCIA inapanga kumsajili golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa Manchester City, David Silva mwenye umri wa miaka 34, wote wakiwa ni raia wa Hispania. ***(90min)***



HABARI MICHEZO

# MWENYEKITI NAMUNGO ASHTUSHWA NA KIPIGO

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kucheza mechi 20 bila kupoteza, rekodi ya Namungo FC, ilivunjwa Jumatano ilipokubali kipigo cha paka mwizi cha mabao 3-0 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza na kuwashtua viongozi wa timu hiyo.

Mwenyekiti wa klabu ya Namungo, Hassan Zidadu, amesema kuwa ameshtushwa na kipigo hicho na kusema hajui nini kimetokea.

"Nilipoangalia matokeo hayo nilishtuka kidogo, sijazungumza na kocha na nahodha wa timu kujua kuna nini kimetokea, nadhani baadaye nitafanya hivyo nao watanimbia... lakini kiukweli si jambo la kawaida na ni vigumu sana kumwambia mtu eti Namungo imefungwa mabao 3-0 na Mbao FC," alisema mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, alisema ingawa hajazungumza na kocha, lakini inawezekana wachezaji wake walikuwa wakicheza kwa tahadhari kujilinda kuumia ili wasikose mechi yao dhidi ya Simba, Agosti 2 kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga kwenye fainali ya Kombe la FA.

"Nadhani wachezaji fikra zao ziko kwenye fainali, ila kwa hali ya kawaida kila mtu anashangaa kwa Mbao ilivyo na Namungo ilivyo halafu eti tumefungwa mabao 3-0, ni ngumu na ajabu," alisema Zidadu.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Namungo, Hitimana Thiery, alisema kuwa mchezo ulikuwa mgumu kwa sababu wachezaji wake walikuwa wakicheza kawaida wakiwa hawana cha kupoteza, huku wenzao wa Mbao FC wakicheza kama fainali yao, kwa sababu walikuwa wanataka washinde ili kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

Namungo imehitimisha mwendelezo wao mzuri wa kucheza bila kufungwa, kwani ilicheza mechi 20 bila kupoteza.

Mara ya mwisho ilipocheza Januari 29, ilipochapwa mabao 3-2 dhidi ya Simba na baada ya hapo ikacheza mechi 20 bila kupoteza ikishinda mechi 7 na sare 13.



Mshambuliaji wa timu ya KMC, Ramadhan Kapera (kushoto), akiwania mpira wa juu na mchezaji wa Tanzania Prison, Nurdin Chona, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Katwila ana siri kubwa Mtibwa kufanya vibaya

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuber Katwila, ana siri kubwa juu ya kufanya vibaya kwa timu yao na amesema kwa sasa anawaanda kisaikolojia na utulivu wachezaji wake, ili kutafuta pointi tatu katika mechi yao ya mwisho ya kumalizia Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema sasa hawezi kuweka wazi matatizo ya timu yake kwa sasa anapigania kutafuta pointi muhimu katika mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting.

Alisema baada ya ligi kumalizika ataweka wazi sababu ya wao kutofanya vizuri hali inayosababisha kupambana kujinasua katika nafasi mbaya waliyokuwapo.

"Kwa sasa siwezi kusema chochote sababu tuna mechi moja tunahitaji kupambana kutafuta pointi, sasa nawaandaa wachezaji wangu saikolojia na kuwa watulivu ili tupate alama hizo tujiweke katika nafasi nzuri," alisema Katwila.

Alisema bila ya kuwajenga kisaikolojia na utulivu wachezaji wake watakuwa na wakati mgumu katika mechi yao ya mwisho.

Katwila alisema ana imani ya kupata matokeo katika mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting kwa kujikusanyia pointi tatu muhimu na kuiweka timu hiyo katika nafasi nzuri.

"Hii mechi ni muhimu sana kwetu tunahitaji utulivu wa hali ya juu kupata pointi na kujiweka katika nafasi nzuri, suala la kushuka daraja haliwezekani tunaenda kupambana," alisema Katwila.

Mtibwa inahitaji pointi tatu ili ijikusanyie jumla ya pointi 45 ambayo kwa sasa ipo nafasi ya 14 ikiwa na alama 42 wakia chini ya Mwadui FC yenye alama 44 wakiwa nafasi ya 13, huku KMC wakiwa na pointi 46 katika nafasi ya 12 katika msimamo wa Ligi Kuu.

## Minziro awaita wana Mbao kuibakiza Ligi Kuu

Na Faustine Feliciane

BAADA ya ushindi wa sita mfululizo katika michezo saba iliyocheza hivi karibuni, kocha wa Mbao FC, Felix Minziro, amewataka mashabiki wa timu hiyo kujazana kwa wingi uwanjani Jumapili kushuhudia timu hiyo ikijihakikishia kubaki Ligi Kuu.

Mbao juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 mbele ya Namungo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Minziro, alisema kuwa ushindi huo ni chachu kuelekea kwenye mchezo wao wa mwisho dhidi ya Ruvu Shooting utakaochezwa Jumapili kwenye uwanja huo.

"Nimefurahia sana matokeo tuliyoyapata jana (juzi), lakini nimewaambia wachezaji kazi bado haijaisha, mashabiki nawaomba waendelee kujitokeza na kujazana uwanjani kuendelea kutusapoti ili kuhakikisha tunapata ushindi utakaotuhakikishia kubaki Ligi Kuu," alisema Minziro.

Aidha, alisema kuwa nafasi ya 16 wanayoishika sasa (kabla ya michezo ya jana) bado haijawahakikishia kwa asilimia miamoja kubaki Ligi Kuu.

"Mchezo wa mwisho ndio muhimu zaidi kwetu, huo utatuhakikishia kubaki

Ligi Kuu kama tutapata ushindi, ninachosisitiza Wanambao na Wanamwanza kwa jumla kutusapoti kwenye mchezo huu wa mwisho," alisema Minziro.

## Mafunzo yaifungia kazi Jang'ombe

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Mafunzo Said Kwimbi amesema amejipanga kupata alama tatu katika mchezo wake wa leo dhidi ya Jang'ombe Boys ili timu yake iwe kwenye nafasi nzuri katika msimo wa ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kwimbi alisema Ligi ya Zanzibar hivi sasa ni ngumu kutokana na kila timu inataka kujiweka katika mazingira mazuri ikiwamo zinazoongoza ligi zinataka kujiimarisha kileleni na zile zilizo katika mstari hatari zinajipapatua ili zisishuke daraja.


Alisema kuelekea mchezo wake wa kesho timu hiyo imejiandaa kupata alama tatu muhimu licha ya kuwa mchezo mgumu kutokana na timu inayochezanayo inawachezaji wazoefu katika Ligi Kuu ya Zanzibar.

Alisema wapinzani wao Jang'ombe Boys wanawachezaji wazuri hodari na wenye kupambana, lakini mpira mchezo wa makosa lolote linaweza kutokea katika dakika tisini za mchezo.

Aidha, alisema kuwa katika mchezo huo wa kesho timu hiyo ya Mafunzo itawakosa wachezaji wake wawili kutokana na kupata majeraha katika michezo hii ya ligi ambao ni kiungo wa kati Ali Juma na Ali Othman ambao wamepata majeraha ya paja.

Timu ya Mafunzo ipo nafasi ya tano katika msimamo wa ligi wakiwa na alama 43, huku Jang'ombe Boys bado wakiwa katika mstari hatari wa kushuka daraja wakiwa nafasi 12 na alama zao 32.

Michezo
Ijumaa Julai 24, 2020
Nipashe



Henderson: Ni hisia tamu kulinyanyua kombe la EPL HABARI UK 22



Nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson, akiwa amenyanyua kombe la Ligi Kuu ya England pamoja na wachezaji wenzake baada ya kukabidhiwa juzi Jumatano katika mchezo dhidi ya Chelsea, ambao walishinda mabao 5-3 katika Uwanja wa Anfield, Liverpool, England. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YABANWA MKWAKWANI

## Ni baada ya kugawana pointi katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyojaa ubabe, nguvu muda wote huku...

**Na Somoe Ng'itu, TANGA**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Simba wameendelea kubanwa katika ligi hiyo baada kulazimishwa sare ya bila kufungana na Coastal Union katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana.

Kwa matokeo hayo Simba inayofundishwa na Mbelgiji Sven Vandenbroeck imefikisha pointi 85 wakati wenyeji Coastal Union iliyoko chini ya Juma Mgunda wao wamefikisha pointi 53.

Kipindi cha kwanza cha mchezo huo kilimalizika kila upande ukiwa haujaliona lango la mwenzake licha ya kuwa na ushindani muda wote.

Simba alikaribia kupata bao kupitia kwa Shomary Kapombe, lakini beki huyo alipiga mpira pembeni ya nyavu na kupoteza nafasi hiyo ya kufunga akiwa ameshawatoka mabeki wa Coastal Union dakika ya 11.

Coastal Union ilijibu shambulizi hilo kupitia kwa Issa Abushehe, lakini beki mkongwe wa Simba, Erasto Nyoni aliwahi kuokoa hatari hiyo kwenye lango lake dakika ya 18, huku golikipa Aboubakar Abbas akidaka shuti la Kapombe aliyemalizia kazi nzuri ya Miraji Athumani dakika tano baadaye.

Kipa wa Simba, Benno Kakolanya alifanya kazi nzuri ya kusaka shuti la Ayoub Lyanga ambaye hata hivyo alishindwa kupiga vema mpira baada ya kubanwa na Paschal Wawa na kuwanyima Coastal Union goli dakika ya 28 huku Kakolanya tena akidaka kirahisi shuti jepesi lililopigwa na Mtende Juma dakika ya 34.

Coastal Union watalala wanaiota nafasi walipopoteza Lyanga akiwa amebaki peke yake na Kakolanya kwa kupiga juu dakika ya 42 wakati mabeki wa Simba wameshapotea kwenye safu yao la ulinzi, huku mabingwa hao wa Bara wakikosa goli baada ya Ibrahim kupangua mpira wa frikiki iliyopigwa dakika ya 44 na Wawa.

Kipindi cha pili pia kilianza kwa kasi lakini Simba ilipoteza nafasi nyingine ya kufunga baada ya beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto kutoa mpira haraka na kuwanyima nafasi ya kufunga, Muzamiru Yassin dakika ya 54 wakati Kakolanya akiokoa shuti la Hance Masoud dakika ya 65.

Kagere alikaribia kuongeza idadi ya mabao, lakini shuti alilopiga liligonga mwamba na kurudi uwanjani huku mpira uliowahiwa na Nyoni ukidakwa na kipa Ibrahim dakika ya 79.

Hata hivyo Simba ilimaliza pungufu katika mechi hiyo baada ya beki wake, Wawa kuonyeshwa kadi nyekundu ikiwa ni njano ya pili na mwamuzi, Ludovick Charles kutoka jijini, Mwanza.

Mechi nyingine zilizochezwa jana Alliance FC imetoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, huku Polisi Tanzania ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Mjini Moshi, na Lipuli FC imeifunga Ruvu Shooting bao 1-0.

**KAGERE APOKEA TUZO**

Kabla ya mchezo huo kuanza, Kagere alipokea tuzo ya Mchezaji Bora wa Machi kutoka kwa Naibu Waziri Wizara ya Maji, Jumaà Awesu na Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Steven Mguto.

Mshambuliaji huyo Mnyarwanda ndiye anaongoza kwa kupachika mabao kwenye Ligi Kuu msimu huu, akiwa amefunga magoli 22.

**Coastal Union;** Aboubakar Abbas, Hassan Kibailo, Hance Masoud, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Ame, Salum Salum, Mtende Juma, Ayoub Lyanga, Mudathir Said/ Shabani Khamisi (dk83), Ayoub Semtawa na Issa Abushehe/ Issa Kanduru (dk 69).

**Simba;** Benno Kakolanya, Shomary Kapombe, Mohammed Hussein, Erasto Nyoni, Paschal Wawa, Jonas Mkude, Hassan Dilunga, Muzamiru Yassin, Meddie Kagere, John Bocco/ Clatous Chama (dk 67) na Miraji Athumani/ Deo Kanda (dk 67).

# EYMAEL AKERWA, KATWILA KUJIUZULU

**Na Isaac Kijoti, MOROGORO**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, akieleza kutofurahishwa na matokeo ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, Mwalimu wa 'Wakata Miwa' hao, huku Zuber Katwila amesema yupo tayari kujiuzulu kuinoa timu hiyo.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri juzi, Mtibwa ilitangulia kupata bao dakika ya 28 kipindi cha kwanza kupitia kwa Haruna Chanongo akiitendea haki krosi ya Salum Kibimbwa kabla ya Adeyun Saleh kuisawazishia Yanga dakika ya 83.

Matokeo hayo yanaifanya Mtibwa kufikisha alama 42 katika nafasi ya 14 kabla ya mechi za jana, hivyo kulazimika kusubiri hadi mechi ya mwisho dhidi ya Ruvu Shooting kujua hatima yake kubaki ama kushuka daraja.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Katwila alisema hajafurahishwa na mwenendo wa timu yake msimu huu na matokeo iliyoyapata hivyo anaweza kujiuzulu.

"Nipo tayari 'ku-resign' (kujiuzulu) kwa sababu ya matokeo mabaya, kama kocha ninatakiwa kuiongoza timu kushinda," alisema Katwila ambaye ameweka rekodi ya kuibebesha Mtibwa Kombe la Mapinduzi akiwa mchezaji na baadaye kocha.

Kwa upande wake Eymael, alisema hakufurahishwa na matokeo ya sare na kwa sasa wanajipanga kuweza kupata ushindi katika mechi ya mwisho dhidi ya Lipuli FC Jumapili.

Alisema lengo lao ni kushinda mchezo huo, ili kuweza kumaliza nafasi ya pili wakati huu wakiwa na alama 69 tatu mbele ya Azam FC kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Mbeya City.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >